SUPA JACKPOT
TZS. 1,112,462,859
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

## MITAALA MIPYA
Msingi mwisho darasa 6, kusoma sekondari lazima




Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumatano Mei 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581306
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardi...

UKURASA 11

## MCHAKATO KATIBA MPYA WAANZA

# Sheria zote zinazohusu uchaguzi kupitiwa





Jenista Mhagama Tundu Lissu

UKURASA 2

## Lissu atinga polisi, akagua gari lake lenye matundu 30 ya risasi

UKURASA 3



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Jiji la Arusha, wakizima moto uliotokana na mlipuko wa mitungi ya gesi katika kiwanda kidogo cha mikate cha Haji's, katika Kitongoji cha Keranyi wilayani Arumeru jana. Watu wanne walijeruhiwa akiwamo mmiliki wa kiwanda hicho. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

UKURASA WA 4

### MKUTANO USALAMA SADC WATOA MSIMAMO MAPIGANO YA CONGO



RAIS Samia Suluhu Hassan, amehudhuria mkutano wa dharura wa kujadili hali ya usalama wa Mashariki mwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia...

UKURASA WA 5

### WAZIRI: USHOGA UTAATHIRI UKUAJI WA UCHUMI WA NCHI

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima...

UKURASA WA 17

### ACT-WAZALENDO YAONA UPUNGUFU BAJETI KILIMO

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema hakiridhishwi na usimamizi wa sekta ya kilimo na kumtaka Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kuweka wazi mikakati ya...

## Aoza vidole kwa kudungwa sindano ya UTI duka la dawa

UKURASA 3

MICHEZO NABI AONYA, MARUMO IKIAPA KULA NA MAYELE UK. 24

KATUNI UK. 6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitazama vito katika maonyesho ya madini kabla ya kufungua kongamano la wachimbaji madini na mkutano mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA), jijini Mwanza, jana. Kushoto ni Farida Peter na Khadija Ashibaye (wapili kushoto) wote wakiwa ni wachimbaji madini wanawake. **PICHA: OWM**

# Sheria zote zinazohusu uchaguzi kupitiwa upya

**Waandishi Wetu**

SERIKALI imesema kuwa inatarajia kuwasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria zote zinazohusu uchaguzi ikiwa ni maandalizi ya mchakato wa Katiba mpya kabla ya mwaka wa fedha 2022/23 kwisha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda aliyetaka kujua lini serikali itapeleka sheria ya vyama vya siasa, ili mchakato wa Katiba ujulikane utaanza na itatumia mbinu gani kuhakikisha Katiba inashirikisha watu wote.

Akijibu swali hilo, Waziri Mhagama, alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekubali mapendekezo ya kikosi cha Baraza la Vyama vya Siasa na wadau wengi kuhakikisha mchakato wa Katiba mpya unaanza na kuhuisha na kutungwa kwa sheria zinazohusu uchaguzi nchini.

Alilihakikishia Bunge kwa kuzingatia maelekezo ya Rais Samia tayari baraza hilo linashirikiana na wadau kuweka mpango kazi kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na ofisi nyingine zinazohusika, ili kuhakikisha kabla mwaka huu, sheria zote zinazohusu uchaguzi Bunge lipate nafasi ya kuzipitia, kuzitunga na kuzifanyia marekebisho kama italazimika kufanya hivyo.

"Niwahakikishie serikali imezingatia maoni hayo na tayari imejipanga kwa utekelezaji wa mbadiliko ya sheria hizo,"alisema.

Awali, katika swali la nyongeza, Mbunge wa Chumbani (CCM) Ussi Salum Pondeza alihoji serikali imejipanga kutoa elimu kuhusu Katiba mpya na endapo itaanza upya mchakato wa Katiba au itaendelea na rasimu ya Katiba iliyokuwepo katika mchakato wa awali wa Katiba mpya.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Pauline Gekul alisema tayari serikali imeweka bajeti kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu Katiba ya sasa ya mwaka 1977 pamoja na Katiba ya Zanzibar.

Aidha, alisema wananchi wote waliotimiza umri wa miaka 18 na kuendelea watashiriki katika kutoa maoni yao ya mchakato huu mpya wa Katiba, ili ambao hawakutoa maoni awali kwa kigezo cha umri nao wapate fursa ya kufanya hivyo.

Katika swali la msingi, Mbunge Pondeza alitaka kujua ni lini hatua iliyobaki katika mchakato wa kupata Katiba mpya itakamilishwa baada ya kupitishwa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema Rais Samia kwa kutambua umuhimu wa mchakato huo aliunda kikosi kazi kilichoongozwa na Prof. Rwekaza Mukandara ambacho pamoja na na mambo mengine ilikuwa ni kuhuisha mchakato wa Katiba mpya.

"Katika hilo, kimetoa mapendekezo ya hatua sita za kufanywa katika kukamilisha mchakato huu kuwa ni

kuwepo kwa mjadala wa Kitaifa wa kupata muafaka wa masuala ya msingi, kuhuisha sheria ya mabdiliko ya Katiba, kuundwa kwa jopo la wataalamu wa kuandaa rasimu ya Katiba, rasimu ya Katiba kupitishwa na Bunge, kutoa elimu ya uraia na Katiba kupigiwa kura,"alisema.

Mwishoni mwa wiki, Rais Samia alikutana na viongozi wa serikali wanaoratibu mchakato wa Katiba mpya, na kumwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kuitisha kikao maalum cha Baraza la Vyama vya Siasa, ili kuwashirikisha wadau kufanya tathimini ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi kilichoratibu maoni ya watu kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini.

**WADAU WAFUNGUKA**

Mchambuzi wa Masuala ya Siasa, Deus Kimbamba, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kwa kuona umuhimu wa kurejea katika mchakato wa Katiba mpya ili kuukamilisha.

"Kuna watu wana msimamo, tuanze upya. Ili ujue tunaanzia wapi lazima ujue tuliishia wapi, tulikoishia kisheria, tuliishia kwenye Katiba Inayopendekezwa, iliyotokana na Bunge Maalum la Katiba, chini ya Uenyekiti wa marehemu Samuel Sitta (aliyekuwa Spika wa Bunge wa Mstaafu).

"Kama unazungumza tu kisheria, tunaweza kusema basi tuchukue, ile Katiba iliyotokana na Bunge ikapigiwa kura ya ndio au hapa ili izaliwe Katiba mpya.

"Lakini ukiacha mambo ya kisheria, kuna suala la uhalali. Ili kitu kiwe halali hakihitaji tu kiwe kimepitia mchakato wa sheria. Lazima kiwe na ukubalifu. Ukichukua Katiba inayopendekezwa, haina ukubalifu wa watanzania," alisema Kibamba ambaye pia ni Mjumbe wa Taasisi ya Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA).

Kibamba alisema maoni yaliyotolewa na wananchi wamesema hawaikubali Katiba inayotokana na Bunge Maalum la Katiba na wanayoikubali ni Rasimu iliyotokana na Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Joseph Warioba.

Alisema hata wakati wa serikali ya awamu ya sita ikiwa madarakani ambayo Katiba haikuwa kipaumbele, wadau walikuwa wakisema, kama ikitokea mchakato wake ukaanzishwa, pa kuanzia lazima pasiwe ile Katiba Inayopendekezwa kwa kuwa wananchi wengi hawaikubali.

"Wala kisheria huwezi kuanzia kwenye Rasimu ya Jaji Warioba kwa sababu ilishamaliza muda wake, kwa kuwa ilitakiwa ikiingia kwenye Bunge Maalum na likizalisha Rasimu nyingine iitwe Katiba pendekezwa basi kisheria ile ya Jaji Warioba ingekuwa imemaliza muda wake," alisema.

Alisema mapendekezo yao kama wadau wa asasi zisizo za kiserikali ni Rais Samia ateue timu ya wataalam kuhusu Katiba ili wakae na Katiba Pendekezwa na Rasimu ya Jaji Warioba, kuona mapungufu yake na kuyaondoa.

**LISSU**

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu alisema kinachoendelea kwenye mchakato wa Katiba mpya ni maneno tu na hakuna vitendo.

Alisema ili wao CHADEMA wamwamini Rais Samia wanahitaji kuona matendo zaidi kuliko maneno katika mchakato huo wa Katiba mpya.

"Suala la Mchakato wa Katiba mpya bado ni 'bra bra' tunacho hitaji kuona hivi sasa ni vitendo siyo maneno na vikao vinavyoendelea kila siku,"alisema Lissu.

**Imeandikwa: Augusta Njoji na Paul Mabeja (DODOMA) na Romana Mallya**

# Lissu atinga polisi, akagua gari lake lenye matundu 30 ya risasi

**Na Waandishi Wetu**

BAADA ya miaka sita tangu Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Tundu Lissu, kushambuliwa kwa risasi na watu wasiojulikana Septemba 7, 2017, jana kwa mara ya kwanza alifika Kituo Kikuu cha Polisi Dodoma kuliona gari lake lililokuwamo ndani wakati akishambuliwa.

Lissu alifika kituoni hapo kwa ajili ya kuliona gari hilo ikiwa ni sehemu ya mchakato wa kuanza taratibu za kuliondoa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo katika eneo ambalo gari hilo limeegeshwa, alisema kwa mara ya kwanza tangu aliposhambuliwa ameliona gari lake, huku akiliomba Jeshi la Polisi kuendelea kumsaka aliyehusika na shambulio dhidi yake ili ashughulikiwe kwa mujibu wa sheria.

"Nilifanya mawasiliano na uongozi wa Jeshi la Polisi Dodoma. Nashukuru wameniwezesha kuliona nimehesabu matundu ya risasi yako 30. Imenifikirisha sana kwamba risasi zile zilielekezwa kwa mtu mmoja na ni unyama wa hali ya juu,"alisema huku akionyesha kusikitika.

Aidha, Lissu alisema baada ya kukamilisha kuwasilisha nyaraka muhimu, atalichukua gari hilo ili maisha mengine yaendelee.

Kuhusu uvumi kuwa Polisi walilizuia gari hilo, Lissu alisema ni uongo na hakuna siku amekatazwa kuliona gari lake.

"Kuchukua hii gari si kwamba naondoa au nafuta kesi. Kulingana na sheria za Tanzania, kesi za aina hii zinahesabika kama jinai. Kesi hizi huwa mali ya Jamhuri, mimi sina uwezo wa kuamua kesi ifanyike au isifanyike. Mimi natumika kama shahidi tu," alisisitiza.

Kadhalika, mwanasiasa huyo machachali nchini alikanusha tuhuma za kukataa kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kuhusu kushambuliwa kwake ambapo amedai kuwa hajawahi kufanya hivyo kwani anaelewa hilo ni kosa la jinai na halikubaliki kisheria.

"Puuzeni maneno ya kijingajinga siku zote nimekuwa nikitoa ushirikiano kwa polisi na hadi sasa natamani huyo aliyenipiga risasi zote hizo atafutwe na ashughulikiwe kisheria,"alisema.

Kuhusu kuingia na kutoka nchini mara kwa mara, alisema ni kawaida yake na kuwa hali hiyo isichukuliwe kama ni hofu ya usalama wake.

"Nafanya kazi na mashirika ya kimataifa. Safari zangu zipo vilevile kama ilivyokuwa mwanzo. Jumamosi iliyopita nilitoka Ulaya na mwezi ujao nitaenda mara mbili Ulaya. Hiyo ni kawaida na isichukuliwe tofauti," alifafanua.

Alipoulizwa mahali aliko dereva ambaye alikuwa naye wakati anashambuliwa, Lissu alisema yuko Ubeligiji ambako alipelekwa huko kutokana na sababu za usalama wake kuwa kwenye shaka.

"Dereva wangu nilienda naye Ubeligiji, amesomeshwa huko na kujua lugha mpaka ananishinda mimi. Maneno ya kusema amekimbia nchi yake ni ya kijinga muda wowote akitaka atarudi hapa ni kwao,"alisema Lissu.

**Imeandikwa: na Paul Mabeja (DODOMA) na Christina Mwakangale (Dar)**

# Mkutano usalama SADC watoa msimamo mapigano ya Congo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amehudhuria mkutano wa dharura wa kujadili hali ya usalama wa Mashariki mwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), uliotoa wito kwa vikundi vyenye silaha kusitisha uhasama na kujiondoa bila masharti.

Kwa mujibu taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, mkutano huo umefanyika jana mjini Windhoek, nchini Namibia na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

Yunus alisema umehusisha wakuu wa nchi na serikali za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Troika na nchi zinazochangia Vikosi vya Jeshi vya Force Intervention Brigade (FIB).

"Mkutano huu umetoa tena wito kwa vikundi vyenye silaha kusitisha uhasama na kujiondoa bila masharti katika maeneo wanayoyashikilia nchini humo.

"Umewasihi wanachama wa SADC kuunga mkono serikali ya DRC na kushughulikia hali ya usalama ya Mashariki mwa nchi hiyo kabla ya Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Desemba, mwaka huu," alisema.

Alisema umesisitiza uungwaji mkono wa DRC katika mapambano dhidi ya makundi ya kijeshi Mashariki mwa nchi hiyo ili kuleta amani endelevu, usalama na ustawi kwa wananchi wa Congo na Jumuiya ya SADC kwa ujumla.

Alisema mkutano huo umeidhinisha kupeleka kikosi cha Jeshi la SADC kutoka katika Kikosi cha Kudumu cha Jumuiya hiyo ili kuiunga mkono DRC iweze kurejesha amani na usalama.

Pia mkutano huo, umehudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingo; Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa na Rais wa DRC, Fé lix Antoine Tshisekedi.

Wengine ni Waziri wa Mahusiano ya Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Angola, Balozi Téte António; Waziri wa Ulinzi wa Jamhuri ya Malawi, Harry Mkandawire; pamoja na Balozi wa Zambia nchini Namibia, Stephen Katuka.



Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillius Wambura, akibadilishana nyaraka na Mwakilishi wa Koica Tanzania, Manshik Shin jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini mikataba ya askari wa Tanzania na askari wa Korea kushirikiana kwenye mafunzo ya miaka mitatu ya kujijengea uwezo wa kipelelezi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Sirro kuagwa leo baada ya kustaafu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Nchini linatarajia leo kumuaga rasmi aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, ambaye kwa sasa ni Balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe.

Kwa mujibu wa taarifa ya jeshi hilo iliyotolewa jana, kupitia kwa msemaji wa jeshi hilo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime, Sirro amestaafu utumishi ndani ya Jeshi la Polisi kwa mujibu wa sheria Machi, mwaka huu.

Misime alisema sehere hizo zitafanyika katika Chuo cha Taalum cha Polisi Dar es Salaam (DPA) Kurasini kwa gwaride maalum la kumuaga ikiwa ni utaratibu wa jeshi hilo kuaga viongozi waliofikia cheo cha Kamishna na Inspekta Jenerali wa Polisi.

"IGP mstaafu Balozi Sirro amelitumikia Jeshi la Polisi kwa miaka 30 tangu Februari mwaka 1993, alipojiunga rasmi hadi kustaafu Machi, mwaka 2023.

"Ni Mkuu wa Jeshi la Polisi wa 10 kuliongoza jeshi hili tangu Uhuru na ameliongoza kuanzia Mei 28, 2017 hadi Julai 20, 2022 na kupata mafanikio makubwa kwenye mapambano dhidi ya uhalifu na wahalifu ikiwamo kukomesha vitendo vya mauaji yaliyokuwa yakitokea wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani na maeneo mengine pamoja na kupunguza uhalifu," alisema Misime.

Aliwataja wakuu wa Jeshi la Polisi waliomtangulia na miaka waliyoongoza kwenye mabado kuwa ni; Elangwa Shaidi (1964-1970), Hamza Azizi (1970-1973), Samweli Pundugu (1973-1975) na Philemon Mgaya (1975-1980),

Wengine ni Solomon Liani (1980-1984), Harun Mahundi (1984-1996), Omari Mahita (1996-2006), Said Mwema (2006-2013) na Ernest Mangu (2023-2017).

# Asasi yakoleza moto mchakato Katiba Mpya

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Foundation for Civil Society (FCS), limeanza rasmi mbio za mchakato wa Katiba Mpya kwa kuziwezesha asasi za kiraia kufikia sauti za wananchi moja kwa moja.

Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Francis Kiwanga, alisema hayo wakati wa kutia saini hati ya makubaliano ya ushirikiano ya Sh. bilioni 4.9 na Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Umoja wa Asasi za Kiraia (TANGO) uliofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) kwa lengo la kuongeza wigo wa wananchi kushiriki katika utawala bora.

Alisema awali mchakato huo wa katiba ulikwama kwa sababu ya wanasiasa kuubeba na kuacha sauti za wananchi, hivyo watahakikisha wanachukua mawazo, fikra na maoni yao yanaonekana kwenye katiba mpya.

"Suala la Katiba si la mara moja, fahamu kabisa kuna kuelimisha wananchi ambalo tunaanza nalo hatutaki kufanya makosa tuliyofanya pamoja na mkwamo tulipata nyuma moja ni kuchukuliwa na wanasiasa moja kwa moja. Wananchi walioshiriki hawakuwa na nguvu, hivyo tunataka nguvu ya wananchi ionekane kuanza sasa," alisema.

Kiwanga alisema katiba hiyo ni kwa ajili ya Watanzania ambao wana matamanio makubwa ya namna gani taifa liendeshwe, hivyo mawazo na fikra na maono yao kuhusu mama Tanzania yataonekana kupitia katiba.

Alisema kuna masuala ya uwajibikaji, tunu za taifa na utawala bora ambayo yamebebwa na katiba mpya.

"Kuna masuala yanatutatiza sasa hivi hivyo yanatakiwa kupatia ufumbuzi kupitia katiba mpya ili kufahamu haki zao na ni mradi mkubwa sana wa miaka mitatu ambao hata kama tutajitahidi tupate katiba ndani ya mwaka mmoja, kazi kubwa bado itaendelea ya kuelimisha wananchi," alisema.

Mchakato huo, alisema unaanza wakati ambao mchakato ulifanyika bila kuwa na mafanikio ambao ulianza na Tume ya Mabadiliko ya Katiba, maarufu kama Tume ya Warioba na Bunge la Katiba lakini mwafaka haukufikiwa.

"Tunashukuru kwa sasa uongozi uliopo chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwa na utashi wa kisiasa kuona kuna mambo mengi hayapo sawa na inabidi yarekebishwe kupitia katiba mpya," alisema.

Alisema kiasi cha fedha walizopata kitaanza kutekeleza mpango huo na wanashirikiana na taasisi hizo katika mikoa yote nchini na wanatarajia kutia saini mkataba na taasisi zingine 12. Alisema lengo kufikia wananchi wote vijijini ili kushiriki moja kwa moja mchakato wa katiba mpya.

Naye Mwakilishi wa TLS, Mackphason Mshana, alielezea kufurahishwa na mpango huo na kwamba kazi kubwa iliyo mbele yao ni kuangalia sheria zote zinazohusu mchakato wa katiba na chaguzi zinazokuja, kuzijengea uwezo asasi kushirikiana na serikali na wadau mbalimbali.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa JUKATA, Bob Wangwe, alisema wamejikita kushirikisha asasi za kiraia na wananchi kushiriki moja kwa moja kwenye mabadiliko ya katiba.

Alisema ziko sheria zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho ambazo ni ile ya uchaguzi hivyo katika kipindi hicho watakuwa wanafanya kazi hiyo ili kuwapo na mabadiliko chanya.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANGO, Adamson Nsimba, alisema watahakikisha Azaki zinakuwa mstari wa mbele kuwa na mahusiano mazuri na serikali ili sauti za wengi ziweze kufika.

Jumamosi Mei 6, mwaka huu, Rais Samia alikutana na viongozi mbalimbali wa serikali kujadiliana namna ya kuwashirikisha wananchi katika mchakato wa Katiba mpya pamoja na marekebisho ya sheria mbalimbali zinazohusu uchaguzi.

Hatua hiyo ya Rais Samia ilikuwa siku chache tangu Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, kutangaza kuanza mchakato wa Katiba Mpya uliokwama.

Rais Samia alimwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi kuitisha kikao cha Baraza la Vyama vya Siasa.

Lengo la kuitishwa kwa baraza hilo linaloshirikisha vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu ni kutathimini utekelezaji wa mapendekezo ya kikosi kazi kilichokuwa kikiratibu maoni ya watu mbalimbali kuhusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Kikosi kazi hicho kilichokuwa kikiongozwa na Mwenyekiti Prof. Rwekaza Mukandala pamoja na mambo mengine, kilipendekeza mchakato wa katiba mpya uliokwama mwaka 2014 kwa hatua ya katiba pendekezwa kufufuliwa.

## Wavuvi wafa maji kwa kuzama ziwani

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAVUVI watatu wamefariki dunia huku watatu wakinusurika kifo baada ya mtumbwi kuzama majini katika Ziwa Victoria eneo la Kijiji cha Nungwe wilayani Geita mkoani hapa.

Tukio hilo lilitokea Mei 7, mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni baada ya maji kuingia katika mtumbwi huo na kuzama.

Akisimulia tukio hilo, Dickson Alphonce ambaye ni manusra katika ajali hiyo, alisema ndani ya mtumbwi huo walikuwamo watu sita, baada ya mtumbwi huo kuanza kuzama, waliamua kujirusha majini kwa lengo la kujiokoa kila mmoja. Alisema yeye na wenzake wawili waliokolewa na wavuvi waliokuwa karibu na watatu walifariki dunia.

Akithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, Mkaguzi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Geita, Wambura Fidel, alisema kutokana na kasi ya maji yaliyokuwa yanaingia kwenye mtumbwi baada ya chombo chao kutoboka, yaliwashinda hivyo kusababisha mtumbwi kuzama.

Fidel aliwataja walipoteza maisha kuwa ni David Maliyatabu (25), Kamuli Mhoja (20), na Faustine Cleophace (28).

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Magembe, alifika eneo la tukio na kutoa pole kwa wafiwa na kuwataka wavuvi kuvaa vifaa vya uokozi pindi wanapokuwa ziwani kwenye shughuli zao za uvuvi.

"Hata kama unajua kuogelea kiasia gani lazima uingie majini ukiwa na vifaa kinga. Hii itawasaidia kujiokoa mnapokuwa majini muda mwingine inawasaidia kuokolewa kutokana na vifaa hivyo kusaidia kuelea kwa muda mrefu," alisema.

# Waziri: Ushoga utaathiri ukuaji wa uchumi wa nchi

## •Asema ni aibu mwanamume kuwa mke

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema vitendo vya ndoa za jinsia moja kama vitafumbiwa macho vitaathiri nguvu kazi na ukuaji wa uchumi wa taifa.

Kunusuru baa hilo, amewataka Watanzania kuvunja ukimya na kukemea vitendo hivyo na kuwalinda watoto wao ambao wapo katika hatari kubwa ya kufanyiwa ukatili huo.

Dk. Dorothy alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na wakazi wa Kijiji cha Mayamaya wilayani hapo kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Familia yatakayofanyika Mei 15, mwaka huu.

Alisema ni aibu kuona wanaume ambao ndiyo wanategemewa kuzalisha watoto, ndiyo wanakubali kuwa wanawake.

"Hatutakiwi kukubali kupokea matendo ya aibu kama haya. Ni kuhatarisha vizazi vyetu. Hawa watoto ambao tunawaona leo tumezaa madume ya mbegu lakini watu wengine haya madume ya mbegu wanayageuza kuwa kitu kingine. Hivyo, tuchunge watoto wetu kama ambavyo tunachunga mifugo yetu," alionya.

Dk. Dorothy alisema utafiti wa ukatili dhidi ya watoto unaonyesha unafanyika zaidi nyumbani kwa asilimia 60 na wanaofanya ni ndugu na jamaa wa karibu na nje ya familia ikiwamo shuleni.

Alisema tatizo kubwa la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ni ukimya na kumalizana miongoni mwa familia na matokeo yake taarifa hazifikishwi katika vyombo vya sheria.

Alisema sababu kuu za ukimya ni kuepuka hatua za kisheria dhidi ya mkosaji, mila na desturi, kuwapo imanai potofu zenye madhara zinazotekelezwa katika baadhi ya familia, uelewa mdogo kuhusu malezi chanya na mawasiliano duni miongoni mwa familia.

"Kipato duni au umaskini miongoni mwa familia kinapelekea wazai na walezi wengi kutotimiza majukumu yao ya msingi ya malezi na kutowatimizia watoto mahitaji ya msingi, hivyo kuyatafuta sehemu nyingine na kujikuta wakifanyiwa ukatili.

Alisema kuwa kwa mujibu wa taarifa ya makosa ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji kutoka Jeshi la Polisi, kwa Januari hadi Desemba 2022, jumla ya matukio ya ukatili kwa watoto yalikuwa 12,163. Kati yake, wavulana ni 2,201 na wasichana ni 9,962.

"Ninapenda kutoa rai kwa wanafamilia na jamii kwa ujumla kutoficha taarifa za ukatili bila kujali aliyefanya kwa kuwa kufanya hivyo kunasambaza tabia hiyo kwenye jamii na aliyeficha naye kuwa kwenye hatari ya kufanyiwa hivyo," alisisitiza waziri huyo.



Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, akizungumza wakati wa mafunzo maalum ya namna ya kuripoti habari za chanjo, kupitia Wizara ya Afya na Mpango wa Taifa wa Chanjo jijini humo jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Serikali yajivunia kufikisha elimu kikokotoo kwa umma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa hadi kufikia Februari 28, 2023 wanachama wa mifuko ya pensheni 71,836 na waajiri 2,927 wamefikiwa na elimu ya kanuni mpya ya mafao ya pensheni (kikokotoo).

Elimu hiyo imetolewa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavangu.

Mbunge huyo alihoji serikali imejipangaje kushughulikia malalamiko kuhusu kikokotoo.

Katambi alisema serikali ilitangaza matumizi ya kanuni hizo kuanzia Julai mosi, 2022 kupitia Gazeti la Serikali namba 357 toleo la Mei 20, 2022 na kanuni hiyo iliandaliwa kwa kuzingatia haja ya kuboresha, kuwianisha mafao ya wanachama na kuifanya mifuko hiyo kuwa endelevu.

"Kwa kutambua wajibu wa kuwaelimisha wananchi hususani waajiri na wanachama wa mifuko pensheni kuhusu kanuni mpya ya mafao ya pensheni, elimu imeendelea kutolewa na mifuko ya pensheni kwa kushirikiana na TUCTA," alisema.

Alibainisha kuwa mifuko hiyo imetoa elimu kwa waajiri hao ambao 318 ni wanaochangia PSSSF na NSSF ni 2,609, huku wanachama 19,656 wa PSSSF na NSSF ni 52,180 na kusisitiza elimu hiyo itaendelea kutolewa kwa kuwa ni sehemu ya majukumu yao ya kila siku.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema suala la kikokotoo kinacholalamikiwa sio elimu ni asilimia inayotolewa kwenye kikokotoo hicho.

"Lini serikali itafanya ujumuishi kutokana na wastaafu kusumbuka wapo waliokuwa NSSF walihamishiwa PSSSF na wanapotaka mafao wanalipwa tofauti tofauti na kusababisha usumbufu, serikali inawasaidiaje," alihoji.

Pia, alihoji kikokotoo hicho kinaonekana kutohusu majeshi mengine.

Akitoa majibu ya maswali hayo, Katambi alisema kwa watumishi ambao awali walikuwa wakichangia kwa asilimia 25 walikuwa wanapata Sh. milioni 44 na pensheni ya kila mwezi alikuwa analipwa Sh. 800,000 na kwa mabadiliko ya sasa yaliyoridhiwa na wadau wote katika asilimia 33 mkupuo umeongezeka kwa mtumishi huyo sasa analipwa Sh. milioni 58.

"Kwa pensheni ya kila mwezi analipwa zaidi ya Sh.700,000 unaona jinsi ilivyo na faida na asilimia 81 wananufaika na mpango huu," alisema.

Alisema faida za mpango huo ni nyingi kuliko hasara na asilimia 81 wananufaika katika kupata mafao ya mkupuo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushoga ni janga, inahitajika nguvu ya ziada

**VITA** ya kupambana na vitendo vya ushoga inahitaji ushirikiano mkubwa kutoka kwenye jamii, taasisi na serikali ili kukomesha vitendo hivyo.

Pamoja na kukemewa, lakini kuna baadhi ya wanaojihusisha kufanya vitendo hivyo, huamua kujitangaza kupitia mitandano ya kijamii na wengine kujionyesha waziwazi.

Inasikitisha kuona vijana wanaotegemewa kuwa viongozi wa baadaye kujiingiza katika janga hilo ambalo hata kwenye vitabu vitakatifu limekemewa.

Hivi sasa kwenye mikutano ya siasa, kwenye nyumba za ibada, mikutano ya shule, suala kubwa linalojadiliwa ni vitendo hivyo viovu vilivyoshamiri nchini.

Badala ya Taifa kuzingatia mambo muhimu ya maendeleo, inabidi ichukue sehemu ya muda kuzungumzia vitendo hivyo ambavyo vinaharibu tunu ya nchi.

Viongozi wa kisiasa na dini wote sasa wameweka nguvu zao kukemea suala hilo ili vijana wa Kitanzania wasiendelee kuangamia.

Kama vitendo hivyo vikiachwa viendelee kushamiri basi hapo baadaye kutakuwa na taifa la hovyo na hata ile dhana ya vitabu vitakatifu vya kuwataka wanadamu wakazaane haitakuwa imetimizwa.

Inasikitisha kuona vijana wa kiume wenye nguvu eti wanatembea barabarani wakiwa wamelegeza mikono na macho.

Hii dhambi aliyeileta nchini anastahili adhabu kubwa, kama sio duniani basi ahera kwa kusababisha ukiukwaji wa uumbaji wa Mungu.

Sasa hivi ukienda maeneo ya ufukweni unaweza kutoa machozi, kwa sababu utashangaa wanaume wanavyokumbatiana ni kama mtu na mke wake au mchumba wake.

Wengi wa vijana wanaharibikiwa kwa sababu ya tamaa ya kuwa na vitu anavyomuona navyo rafiki yake, bila kujua kuwa mwenzake amevipata kwa kufanya kazi kwa bidii.

Akiona kijana mwenzake anaendesha gari zuri au ana nyumba nzuri na ana pesa ya kumwezesha kuishi bila tatizo, na yeye anataka kumuiga kwa kutafuta njia ya mkato.

Ndiyo maana hata kwenye vitabu vitakatifu kuna zile amri kuu kumi na moja wapo inakataza kutamani kitu chochote alichonacho mwenzako.

Amri zile zinatoa mafundisho makubwa na kama waumini wangeyazingatia, haya yanayotokea sasa yasingekuwapo.

Vita hii ina hitaji nguvu ya pamoja kuanzia kwa wazazi nyumbani, jamii inayowazunguka, viongozi wa dini na kimila pamoja na serikali ili kuhakikisha vitendo hivi vinakomeshwa kabisa nchini.

Watoto wanaharibika wakiwa bado wadogo na baadhi yao wazazi wao wanakuja kugundua tayari wakiwa wamekwisha haribika.

Kinachouma zaidi ni kuona baadhi ya watoto hao wanaharibiwa na ndugu wa karibu wanaoaminiwa na wazazi.

Kuna jamii ambayo hata ikiona vitendo hivyo vinatendeka wananyamaza kwa kuogopa kuonekana wabaya. Lakini wakumbuke kuwa leo wanapoona watoto wa wenzao wanaharibiwa, kesho watakuwa wa kwao na watakuja kujuta kwa kutotoa ushirikiano kwa wenzao.


Pia, kuna watu wanaoaminiwa kuwa watoto wakipelekwa kwao watakuwa salama, wamekuwa ndio chanzo cha kuharibu watoto hao.

Imekuwa ngumu sasa kuamini hata ndugu wa karibu kuwa na mtoto wako na ile heshima na kumpa mgeni kulala na watoto chumba kimoja imeanza kuondoka kwa kuogopa vitendo hivyo kufanyika.

Vitisho vya watenda makosa hayo, vinasababisha watoto kuogopa kusema ukweli kwa wazazi wao na kubaki wakiharibiwa.

Nguvu ya ziada inahitajika kukomesha vitendo hivi visiendelee kutendeka na kuharibu nguvu kazi ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Kuibuka mchakato Katiba mpya, Rais Samia unaupiga mwingi

**SASA** ni wazi kilio cha wadau hasa wanasiasa waliokuwa wakitamani kufufuliwa kwa mchakato wa katiba mpya kimesikika, hiyo ni kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Miongoni mwa hatua hizo ni kumwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kuitisha kikao maalum cha Baraza la Vyama vya Siasa, ili kushirikisha wadau kufanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi.

Kikosi Kazi hicho ni kile alichounda na kukipa majukumu ya kuratibu maoni ya watu kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini, baada ya kilio cha muda mrefu cha wadau cha kuomba katiba mpya.

Mchakato wa kutaka kuwapo kwa katiba mpya, umepitia hatua mbalimbali ambapo sasa utahusisha pia kushughulikia marekebisho ya sheria mbalimbali zinazohusiana na uchaguzi.

Sheria zinazotajwa ni ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na ya Sheria ya Vyama vya Siasa, ingawa sheria hizo hazikutajwa sura na vifungu vyake, kuna pia vipaumbele katika mchakato huo vikiwa ni maboresho ya sheria za uchaguzi kuelekea uchaguzi ujao mwaka 2024 na wa mwaka 2025.

Binafsi ninachukulia uamuzi huo wa Rais kama njia ya kutelekeza nguzo nne ambazo ameshaweka wazi kwamba katika uongozi wake atazisimamia kwa ajili ya ustawi wa taifa hili na watu wake.

Nguzo hizo ambazo amewahi kuzitaja ni maridhiano, ustahimilivu, mageuzi na kujenga upya Tanzania, na kwamba hizo ndizo zinazoweza kuunganisha Watanzania bila kujali tofauti zao za kisiasa.

Baada ya kuchukua nafasi hiyo ya juu katika nchi, ameendelea kusimamia nguzo hizo, kwa ajili ya kuijenga Tanzania mpya inayojali uhuru wa watu, demokrasia, usawa na haki za binadamu.

**Baada ya kuchukua nafasi hiyo ya juu katika nchi, ameendelea**

Kupitia njia hiyo, amefanikiwa kuwaleta Watanzania pamoja bila kujali tofauti zao za kisiasa na kuhakikisha utawala wa sheria, usawa, kutobaguliwa, fursa sawa kwa wote.

Sasa ameruhusu mchakato wa katiba mpya, ili kuhakikisha katika utawala wake, kila mtu anafurahia haki zake za msingi na kutekeleza majukumu yake kwa uhuru kwa mujibu wa sheria bila kubughudhiwa.

Hiyo ni kutokana na kwamba wananchi wamekuwa wakitaka katiba mpya ambayo itakuwa imewekwa haki zao zote za msingi na jinsi ya kuzilinda ili wafurahie matunda ya uhuru wa nchi yao.

Kwa kuwa tangu alipoingia madarakani kilio cha kwanza cha wanasiasa kwake kilikuwa ni katiba mpya hadi akaamua kuunda Kikosi Kazi, ninaamini kwa mchakato unaoendelea watakuwa nyuma yake.

Iwapo watajitokeza wengine kupinga mchakato unaoendelea, ni wazi wanaweza kusababisha ukakwama kama ilivyotokea baada ya Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014.

Nimeelezea hayo kutokana na ukweli kwamba, vipo baadhi ya vyama vya siasa ambavyo havikubaliani na jinsi baraza hilo linavyoendeshwa, ambalo msajili ameelezwa kukutana nalo, kwa ajili ya mchakato huo.

Lakini kwa kuwa lengo la wadau wakiwamo hata CCM ni kuwapo katiba mpya, basi ingekuwa ni vyema wote watakuwa na lengo moja la kuhakikisha katiba hiyo inapatikana, kwa maslahi mapana ya umma.

Kimsingi, mageuzi yanayofanywa na Rais Samia, katika nyanja mbalimbali, yanalenga kuimarisha juhudi za kuelekea kuwa na jamii yenye haki, ustawi wa demokrasia na uchumi unaokuwa kwa faida ya Watanzania wote, hivyo haina budi kuungwa mkono na Watanzania kuanza kutekeleza na kushiriki kila hatua lile serikali inalopendekeza ili kufanikisha uwepo wa katiba mpya na kudumisha demokrasia.

## Vijana 3,000 kunufaika mafunzo ya kibiashara

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya vijana 3,000 wanatarajia kunufaika na programu ya mafunzo ya kujiendeleza kibiashara na mbinu za kufikia masoko wilayani Temeke.

Mafunzo hayo yanatarajiwa kutolewa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Temeke kwa kushirikiana na Kampuni ya TAMAMU kuanzia Mei 20 hadi 24, mwaka huu kupitia tamasha la 'janjaruka'.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mwanahamis Mkunda, alisema lengo la tamasha hilo ni kuhamasisha wafanyabiashara na vijana kujiunganisha na fursa mbalimbali za kibiashara zinazopatikana katika wilaya hiyo.

"Ninaamini kwamba kupitia tamasha hili la kibiashara, vijana wa Temeke watafahamu fursa mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana katika wilaya hii, watapata pia urahisi wa upatikanaji leseni za biashara, watajengewa uwezo na mbinu za kukabiliana na masoko," alisema Mkunda.

"Watapanua wigo wa biashara hasa ikizingatiwa kuwa halmashauri imekuwa ikitenga asilimia 10 ya mapato yake kuwezesha vikundi vya maendeleo hususani wanawake, vijana na wenye ulemavu lakini hata hivyo wanufaika wengi wamekuwa na biashara za kujirudia na mazoea, kwa hiyo ushiriki wa wazalishaji utasaidia sana kuwaonyesha fursa nyingine ambazo vijana watazitumia."

Mwakilishi wa TAMAMU, James Mgeni, alisema maandalizi ya tamasha hilo yapo katika hatua nzuri na kwamba zaidi ya fursa za kibiashara 800 zitapatikana.

"Kwa hiyo niwakaribishe kwamba tutahakikisha malengo ya kila mdau yanafikiwa, tunawaalika wadau wote wa biashara wenye fursa mbalimbali kwa vijana wetu walitumie vyema tamasha hilo la Janjaruka ili kuongeza na kupanua wigo wa biashara zao katika halmashauri ya Temeke," alisema Mgeni.



Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Zanzibar, Othman Ally Maulid (kushoto), akizungumza kwenye maadhimisho ya Wiki ya Jumuiya ya Wazazi katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Taasisi bunifu Marekani zafurahia uzuri Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI wa taasisi mbalimbali za nchini Marekani hususani wa jiji lenye makao makuu ya taasisi nyingi za ubunifu na teknolojia la Seattle katika jimbo la Washington, wamefurahishwa na uzuri wa Tanzania baada ya kupata fursa ya kutazama sehemu ya filamu ya "Tanzania; The Royal Tour."

Wawakilishi hao wakiongozwa na mmiliki wa klabu ya Ligi Kuu ya Mpira wa Miguu ya Marekani na mabingwa wa Mabara, Seattle Sounders, Adrian Hanauer, ambaye pia ni mwanahisa katika kampuni kubwa ya Amazon, walionekana wakishangilia na kupiga makofi katika sehemu mbalimbali za filamu hiyo, huku wengi wakiahidi kuwa Julai, mwaka huu, watatembelea Tanzania.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni mwanamke wa kwanza katika historia ya nchi yetu kushika wadhifa huo, amejitoa kuwa kama mwongoza watalii na kuionesha nchi yetu kazika filamu hii ya Royal Tour katika namna ambayo haijawahi kutokea. Karibuni sana Tanzania mje kujionea vivutio mbalimbali," alisema Katibu Mkuu-Maliasili, Dk. Hassan Abbas, aliyeko katika ziara ya kikazi mjini humo akiambatana na Damas Mfugale, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

Pamoja na Hanauer, mmiliki wa klabu ya Seattle Sounders, baadhi ya wawakilishi wa taasisi nyingine kubwa na za kimkakati waliohudhuria hafla hiyo na kuitazama filamu ya Royal Tour, ambayo pia ilioneshwa kupitia 'screen' kubwa za Uwanja wa Lumen (moja ya viwanja vitakavyotumika pia kwa fainali za Kombe la Dunia 2026) ni David Young, Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Klabu ya Seattle Seahawks, Andrea Bailey kutoka klabu ya NBA ya Portland Trail Blazers.

Wengine ni Michael Woody, kutoka kampeni ya Visit Seattle, Anbessie Yitbarek, Makamu wa Rais wa Masuala ya Biashara Ukanda wa Afrika kutoka kampuni ya Boeing, Reed Forrester Meneja wa Shirika la Ndege la Delta, AJ Jones II, Ofisa Mwandamizi wa Mawasiliano, kampuni ya Starbucks na Sarah Gavin, kutoka makao makuu ya Google.

# Kesi ya Makonda yaondolewa kortini

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeliondoa shauri la madai namba 234/2022 lililofunguliwa na mfanyabiashara Patrick Kamwelwe dhidi aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na William Malecela, maarufu 'Lemutuz', kwa kuwa mdai ameshindwa kufika mahakamani mara nne mfululizo.

Kutokana na utata wa uraia wa mdai (Kamwelwe) Februari Mosi, 2023, Wakili wa Malecela, Ruben Simwanza, aliiomba mahakama wamtangaze mdai kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa kuwa wameshindwa kumpata.

Mahakama ilifikia uamuzi huo jana baada ya Mawakili wa Makonda, Gift Joshua na Simon Mawala, kuwasilisha ombi la kuliondoa shauri hilo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate wa mahakama hiyo.

Mawakili hao waliiomba mahakama kuliondoa shauri hilo kwa kuwa mdai hajafika mahakamani mara nne mfululizo na pia hata jana mawakili wa mlalamikaji hawakuwapo mahakamani.

Baada ya kusikiliza ombi hilo, Hakimu Ngimilanga alikubali ombi hilo la mawakili wa wajibu maombi na kulifuta shauri hilo namba 234,2022.

Awali, Makonda na Malecela ambaye ni mmiliki wa Blogu ya Lemutuz, walifungua maombi madogo baada ya kuwa na shaka na uraia wa Kamwelwe kwa kutokuwa na mali zinazohamishika nchini, kwa kuwa kisheria anatakiwa kulipa gharama za uendeshaji wa shauri hilo.

Simwanza alidai wameshindwa kumpata mfanyabiashara Kamwelwe. Hivyo, wanaomba mahakama hiyo watangaze katika vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii kwa sababu jitihada zao zimegonga mwamba.

Alidai kuwa, kesi ilivyoitwa Desemba 8,2022 kwa mara ya mwisho wakili anayemwakilisha Kamwelwe, Wabeha Kung'e, alijiondoa kwenye kesi ya msingi na kesi ndogo waliyofungua madai yetu.

Kamwelwe anayeishi jijini New York, Marekani, alifungua kesi ya madai dhidi ya Makonda na Malecela, akiwataka wamlipe fidia ya Sh. milioni 247.2 kwa madai kuwa wamemdhulumu gari lake aina ya Range Rover Sport.

Kamwelwe aliiomba mahakama imwamuru Makonda na Malecela kumlipa kiasi hicho cha fedha kama fidia anayodai kuwa imetokana na hatua ya wadaiwa hao kumdhulumu gari lake jeusi aina ya Toyota Rand Rover/Range Rover Ronge Sport, lenye namba 20153.

Mdai huyo (Kamwelwe) katika hati yake ya madai, alitaka Makonda na Malecela, walimpe dola za Marekani 11,250, kama gharama ya kodi ya kuliingiza gari hilo, dola za Marekani 50,000 za fidia ya kulichukua gari hilo pamoja na dola 45,000, ambayo ni thamani ya gari hilo.

Kamwelwe pia alidai Makonda ameendelea kulitumia gari hilo hata baada ya kuondolewa madarakani licha ya kwamba si mali yake halali.

Katika hati yake ya madai, Kamwelwe anadai mwaka 2017 alifuatwa na Malecela na kumweleza kuwa Makonda anaomba amwazime gari aina ya Range Rover.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wasira ateuliwa msimamizi mazishi ya Nimrod Mkono

**Na Sabato Kasika**

FAMILIA ya mbunge wa zamani wa Musoma Vijijini na Butiama, marehemu Nimrod Mkono, imeunda kamati maalum inayoratibu utaratibu wa kusafirisha mwili wake kutoka Marekani kuja Tanzania.

Kamati hiyo inaongozwa na mwanasiasa mkongwe Stephen Wasira, akisaidiwa na Balozi James Nzagi.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Wasira aliiambia Nipashe jijini Dar es Salaam jana kuwa tangu kutokea msiba huo, kumekuwapo na taarifa nyingi zisizo na ukweli zinazosambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Taarifa hizo zimezusha sintofahamu kwenye familia ya marehemu na hata kwa watu wengi wanaompenda, kumheshimu na kumuenzi. Ukweli ni kwamba taratibu za kusafirisha mwili zinaendelea vizuri kwa kushirikiana na familia na ubalozi wa Tanzania jijini Washington DC," alisema Wasira.

Bila kufafanua, alisema kamati hiyo inauhakikishia umma kuwa hakuna mgogoro wowote wa kifamilia kuhusu msiba huo na kwamba familia imepanga mwili uzikwe nyumbani kwa marehemu, Kigori Busegwe, Wilaya ya Butiama, mkoani Mara.

"Tarehe ya kuletwa mwili itatangazwa. Baada ya hapo, ratiba kamili itatolewa ili kuwawezesha ndugu, jamaa na marafiki walio ndani na nje ya nchi kushiriki kikamilifu katika maziko," alisema.

Wakili Mkono alifariki dunia Aprili 18, mwaka huu, nchini Marekani alikokuwa akitibiwa.



Mwanafunzi wa Shule ya Kimataifa ya Feza, Haris Magesa (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, baada ya kuibuka mshindi wa tatu wa mashindano ya Hisabati ya Afrika Mashariki na kukishukuru Chama cha Hisabati (MAT/CHAHITA) kilichopo Idara ya Hisabati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinachosimamia mashindano hayo nchini. Kushoto ni Baba wa Haris, Phares Magesa na mama yake, Haika Lawere. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Barua makubaliano kesi ya JATU utata

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya JATU Public Ltd, Peter Gasaya (32), anayetuhumiwa kujipatia Sh. bilioni 5.1 kwa njia ya udanganyifu umeieleza mahakama kuwa haujapata barua ya makubaliano 'plea bargaining' ya mshtakiwa.

Hayo yalidaiwa jana na Wakili wa Serikali, Agness Mtungunja, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Pamela Mazengo, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

Mtungunja alidai kuwa hawajapata barua plea bargaining, kwa hiyo wanaomba muda wafuatilie kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kama barua hiyo imefika. Hata hivyo, Wakili wa mshtakiwa, Kung'e Wabeya, alisisitiza barua hiyo ya kuingia makubaliano ya kumaliza kesi hiyo alishaipeleka kwa DPP.

Baada ya wakili kudai hayo, Hakimu Mazengo aliahirisha kesi hiyo ambayo ilikuwa ikiendeshwa kwa njia ya mtandao 'Video Conference' hadi Mei 22 kwa kutajwa.

Ilidaiwa katika shtaka la kwanza mshtakiwa anatuhumiwa kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba 31, 2021 jijini Dar es Salaam, akiwa Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo kwa njia ya udanganyifu alijipatia Sh. 5,139,865,733 kutoka Saccos ya JATU.

Gasaya anadaiwa kujipatia fedha hizo kwa njia ya udanganyifu kutoka Saccos ya JATU kwa kujipambanua kwamba fedha hiyo ataipanda kwenye kilimo cha mazao, jambo ambalo alijua kuwa sio kweli.

Katika shtaka la pili la kutakatisha fedha, tarehe hiyo akiwa mtendaji mkuu na mwanzilishi wa JATU Saccos, alijihusisha na muamala wa Sh. 5,139,865,733 kutoka katika akaunti ya Saccos hiyo iliyopo benki ya NMB tawi la Temeke kwenda katika akaunti ya JATU PLC iliyopo katika benki ya NMB tawi la Temeke.

Mshtakiwa anatuhumiwa kuwa alifanya hivyo wakati akijua fedha hizo zinatokana na kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

## Maeneo yote yaliyokumbwa mafuriko yafanyiwa tathmini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira imejipanga kufanya tathmini ya kina katika maeneo yote yanayokumbwa na mafuriko nchini ikiwamo Jimbo la Mwera.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Hamza Khamis Chilo, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mwera (CCM), Zahor Mohamed Haji.

Mbunge huyo alihoji mkakati gani wa kudhibiti mafuriko ambayo husababisha uchafuzi wa mazingira na kuongeza umaskini katika Jimbo la Mwera.

Naibu waziri alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kufanya tathmini hiyo.

Aidha, alisema katika kudhibiti mafuriko katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Magharibi A'' yakiwamo maeneo ya Jimbo la Mwera, hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni pamoja na kuunda Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya ya Magharibi 'A' yenye jukumu kuu la kuratibu utekelezaji wa Mpango wa wilaya wa kukabiliana na maafa ya mwaka 2022 sambamba na kuwaelimisha wananchi.

"Pia kuandaa mpango wa wilaya wa kukabiliana na maafa ambao umeainisha wadau majukumu yao na mpango wa utekelezaji," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge alihoji kwa muda mrefu wanazungumzia adha ya mafuriko kwenye eneo hilo na kutaka kujua kauli ya serikali lini itashughulikia tatizo hilo.

Chilo alimhakikishia mbunge huwa serikali inatambua tatizo hilo na kupitia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ili kukabiliana nayo.

## Madereva wa BOLT waonywa

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya Usafiri kwa njia ya Taxi-Mtandao (BOLT) imewatahadharisha madereva wake kutofanya shughuli au kujihusisha na mawakala ambao hawajaidhinishwa, wanaodai kuwakilisha BOLT.

Pia, imesema kuanzia sasa itafungia dereva yeyote mwenye viashiria au anayetumia programu haramu.

Meneja Mkazi wa kampuni hiyo, Charles Matondane, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari alisema kutokana na hali hiyo, BOLT inafanya kazi kwa ukaribu na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), ili kuboresha usalama na viwango katika soko la taxi-mtandao.

"Tunashukuru kwa hizi hatua kwani zitaboresha usafiri wa taxi-mtandao kote nchini, na pia kutatua masuala yanayoathiri madereva na jumuiya ya abiria," alisema.

Matondane alisema wana ofisi moja iliyosajiliwa Dar es Salaam na kushauri umma kutofanya shughuli yoyote rasmi na watu wasioidhinishwa.


Pia, alisema wameripoti maeneo mawili katika vituo vya polisi vikuu jijini Dar es Salaam ili kuwachukulia hatua watu hao wasio halali.

Alisema kampuni inafanya kazi na mamlaka husika kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watu wanaodai kuwa mawakala walioidhinishwa kuwasaidia usajili madereva kwenye tovuti au programu ya kampuni.

"Tungependa pia kusisitiza kwamba BOLT haiwatozi kiasi chochote madereva kufanya usajili kwenye tovuti au programu ya kampuni, kwa hivyo, madereva hawapaswi kumlipa mtu yeyote ili kupata huduma ya usajili katika tovuti au programu ya kampuni kwani kampuni haitawajibishwa kwa miamala yoyote kama hiyo," alisema.

"BOLT imetoa taarifa za madereva hao waliofanya makosa hayo LATRA na Kituo cha Polisi Kati kwa hatua zaidi kuchukuliwa dhidi ya madereva hao.

"Tumekuwa tukifanya kazi na kampuni za mifumo ili kuhakikisha programu hizi haramu na udukuzi wa simu janja unapunguzwa ili kuhakikisha takwimu na taarifa zao za GPS hazitarekebishwa ili kupandisha bei ya safari," alisema.





# CRB yakemea rushwa katika utoaji zabuni

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

BODI ya Usajili ya Makandarasi (CRB), imeonya kuhusu rushwa wakati wa ufunguzi wa zabuni na wanapotekeleza miradi mbalimbali kwa kuwa hali hiyo ikiachwa inadhoofisha haki na ufanisi katika kazi wanazopewa wakandarasi.

Mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Joseph Nyamuhanga, alionya vitendo hivyo wakati akifungua mkutano wa mashauriano, baina ya wadau wa ujenzi mkoani Arusha.

"Mkandarasi anayejihusisha na vitendo vya rushwa, wakati wa kuomba au kugawa zabuni ni dhahiri kuwa siyo mzalendo.

"Makandarasi waepuke vitendo vya rushwa wakati wa ufunguaji zabuni na wakati wauetekelezaji wa miradi, lakini pia waungane na wabia katika utekelezaji wa miradi ya ndani," alisema.

Pia aliwashauri kuhakikisha wanawatumia wataalamu katika zabuni wanazopewa ili kuendeleza uaminifu na kuendeleza kutunza weledi wao.

Awali, Msajili wa Bodi hiyo, Rhoben Nkori, alisema mkutano huo umewakutanisha washiriki 270 wakiwamo makandarasi 150 na washiriki wengine ni 100.

"Tatizo ni kuongezeka kwa utitiri wa kodi na mirabaha inayomwongezea mzigo mkandarasi wakati wa utekelezaji wa miradi. Azimio lake ni sheria husika zinazoelekeza utozaji wa kodi uwekwe wazi na viwango vyake viwekwe wazi," alisema Nkori.

**"Mkandarasi anayejihusisha na vitendo vya rushwa, wakati wa kuomba au kugawa zabuni ni dhahiri kuwa siyo mzalendo.**

# Ndalichako ataja kikwazo wanaokwenda kufanya kazi ughaibuni bila utaratibu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amesema uhamaji wa nguvu kazi nchini kwenda nje ya nchi, ndicho chanzo kikuu cha ukiukwaji wa haki za binadamu.

Amesema uhamaji huo usiofuata taratibu rasmi, unaharibu taswira ya nchi kwa kuwa hawazingatii itifaki za Umoja wa Mataifa.

Akizungumza jana jijini hapa katika kikao cha siku tano cha kujadili masuala ya uhamaji wa nguvu kazi kwenda nje ya nchi, Prof. Ndalichako alisema kuna haja ya wadau wanaoshiriki kikao hicho kujadili na kuishauri serikali namna bora itakayotatua matatizo yanayotokana na uhamaji wa nguvu kazi.

Prof. Ndalichako alisema vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa, wamekuwa na mawazo ya kwenda ughaibuni kwa lengo la kutafuta fedha, lakini hali hugeuka na kuwa tofauti.

"Mambo yanapokuwa tofauti wanajikuta wakikimbilia balozi zetu huko waliko na lazima kuwasaidia sababu serikali ndiyo baba na mama. Huwezi kuacha watoto wako wakihangaika," alisema.

Kutokana na tatizo hilo, alisema serikali imeona ni vyema kupitia upya mpango utakaowezesha Watanzania kufuata utaratibu rasmi wa kwenda ughaibuni kutafuta kipato ili kuwaepusha na matatizo wanayokumbana nayo.

"Lakini nashauri katika kikao hiki tutoke na namna bora ya kuishauri serikali jinsi ya kuziba mianya ya njia zisizo rasmi zinazotumika ili kila mmoja anayeenda ughaibuni atumie njia rasmi zinazotambulika ili akipata shida iwe rahisi kusaidiwa,"alisema.

Ndalichako alisema wageni wanaokuja nchini wanafahamika na rahisi kuwaratibu kwa sababu wanaingia kwa kuzingatia mfumo rasmi.

Mshauri Mkuu wa Ufundi wa Mradi wa Usimamizi wa Uhamiaji katika nchi za Kusini mwa Afrika, anayefanya kazi na Shirika la Kazi Duniani ( ILO), Gloria Morenyo, alisema lengo la kikao kazi hicho ni kujenga ujuzi wa namna bora ya kukabiliana na matatizo yanayowakuta nguvu kazi nje ya nchi wanapoenda kufanya kazi.

Aidha, Mwakilishi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Ameir Ali Ameir, alisema ni muhimu kufahamu mikataba yao wanapoenda kufanya kazi nje ya nchi na haki zao za msingi kule wanakokwenda kufanya kazi ili wakipata madhila wasaidiwe kwa urahisi.

Pia alishauri wanaokuja nchini muhimu kuwajua wangapi na wameingia vipi na kubwa kulinda usalama wa nchi, ambao ndio jambo kubwa kuliko chochote.



Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga Bombo, Dk. Juma Ramadhani, akitoa zawadi kwa mmoja ya wagonjwa waliolazwa kwenye hospitali hiyo juzi ikiwa ni kusherehekea maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Kilindi yakabiliwa upungufu walimu 724

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WILAYA ya Kilindi mkoani Tanga, inakabiliwa na upungufu wa walimu 724, sawa na asilimia 43 ya mahitaji, hali ambayo imekuwa ikichangia ufaulu mdogo wa wanafunzi.

Taarifa ya upungufu huo iliwekwa wazi juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Gracian Makota.


Makota alisema hayo alipokuwa akijibu hoja ya Diwani wa Viti Maalum (CCM), Hamida Kidunda, aliyetaka kujua halmashauri imechukua hatua gani kukabiliana na upungufu wa walimu wilayani hapa.

Hamida aliibua hoja hiyo kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani la Wilaya hiyo. Wakati anahitimisha hoja yake, Hamida aliishauri halmashauri kupeleka ombi maalum Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupata upendeleo wa mgawo wa ajira mpya za walimu.

Akijibu hoja hiyo, Makota, alieleza kuwa upungufu wa walimu katika Halmashauri hiyo ni mkubwa, kwa kuwa uhitaji ni walimu 1,652. Kati yao walimu waliopo ni 928 na idadi ya walimu wa kike walioko ni 348.

"Upungufu wa walimu wa kike ni mkubwa lakini uko mpango wa kukabiliana nao hususani kipindi hiki cha ajira mpya za walimu.

"Kwa upande wa shule shikizi, kuna shule 42 zilizopo katika Halmashauri yetu na 15 pekee, ndizo ambazo zimeombewa usajili wa kudumu, baada ya kufanyiwa ukaguzi mdhibiti ubora, kwamba zinakidhi vigezo vya kuwa shule za msingi," alisema.





# Walimu 1,140 wahitajika Maswa

**Na Alex Sayi,** MASWA

WALIMU 1,148 wanahitajika katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaoendelea kudahiliwa kuanza darasa la kwanza kutokana na mpango wa elimu bila malipo.

Katika halmashauri hiyo wanafunzi ngazi ya awali na msingi wameongezeka kutoka 15,174 kwa mwaka 2021/22 mpaka 15,946 kwa mwaka wa masomo 2022/23.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu hali ya elimu ya swali na msingi. Mkuu wa Divisheni ya Elimu Msingi wilayani Maswa, Dk. Lucy Kurogwa, alisema halmashauri kwa sasa ina upungufu mkubwa wa walimu kutokana na ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa sambamba na wale wanaofaulu kuendelea na kidato cha kwanza.

"Tuna jumla ya shule za msingi 135 kati ya hizo, 132 ni za serikali na tatu ni binafsi. Licha ya ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi, ufaulu wa darasa la saba umeongezeka kwa asilimia 95 ikilinganishwa na 84 hapo awali. Hali hii pia imesabibisha upungufu wa walimu 1,148 kati ya walimu 1,109 waliopo kwa sasa huku mahitaji yakiwa ni walimu 2,257," alisema Kurogwa. Kuhusu hali ya miundombinu, alisema elimu ya msingi inakabiliwa na upungufu wa madarasa 930 sawa na asilimia 41 kati ya madarasa 1,327 yaliyopo kwa sasa, upungufu nyumba za walimu 649 sawa na asilimia 58 kati ya nyumba 460. Upungufu matundu ya vyoo ni 3,411 sawa na asilimia 74 kati ya matundu 1,182 yaliyopo kwa sasa na upungufu wa madawati ni 10,980 sawa na asilimia 32 kati ya madawati 22,855.

Naye Fidericy Apolinary, Mkuu wa Divission Elimu Sekondari, alisema kwa sasa kuna ongezeko la shule za sekondari toka shule 40 hadi 45, ikiambatana na ongezeko la wanafunzi kwa asilimia tisa toka wanafunzi 15,673 hadi 17,540, huku ufaulu kidato cha nne ukiongezeka kwa asilimia tatu toka asilimia 92 hadi 95.

"Elimu Sekondari inaendelea vizuri, tunapambana kutokomeza zero kwa ufaulu wa kidato cha nne na tunapambana kukomesha utoro. Hili litawezekana kwa kuwa hali ya miundombinu kwa sasa iko vizuri na tuna madarasa 504 sawa na ongezeko la asilimia 40 ikilinganishwa na madarasa 352 mwaka 2020," alisema Aporinary.

Akizungumza na wananchi na wafanyakazi hivi karibuni mjini Lamadi wilayani Busega mkoani Simiyu, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahya Nawanda, alisema katika sekta ya elimu kumekuwa na kero mbalimbali ambazo kwa sasa zimeanza kutatuliwa.

Alisema fedha ambazo wamekuwa wakipokea kutoka serikali kuu kwa lengo la kuboresha sekta hiyo, zimekuwa zikifika kwa wakati.

"Mbali na Sh. bilioni 126 tulizopokea ndani ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni tumepokea zaidi ya Sh. bilioni tisa kwa ajili ya ujenzi wa matundu 100 ya vyoo, ujenzi wa nyumba za walimu na vyumba vya madarasa," alisema Dk. Nawanda.




Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo wa Kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Salman Karmal (wa nne kulia), pamoja na wachimbaji wadogo wa madini mkoa wa Geita, wakikata utepe kufungua ofisi ya kampuni hiyo ya uuzaji na ukodishaji wa mitambo kwa ajili ya shughuli za migodini katika eneo la soko la dhahabu mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Tabora imemhukumu Kamuga Bujije kunyongwa hadi kufa baada ya kukutwa na hatia ya kuua kwa kukusudia kwa kosa alilotenda Juni 27, 2021.

Wakati Bujije akihukumiwa kunyongwa hadi kufa, wenzake watano wamehukumiwa kifungo cha miaka minane jela na wawili kifungo cha miaka 10 jela kwa kutekeleza mauaji kwa nyakati tofauti bila kukusudia.

Bujije alikutwa na hatia kwa kumuua Mosafa Mpongwa kwa kumkata mapanga kwa wivu wa mapenzi na kuhukumiwa adhabu hiyo ya kunyongwa mpaka kufa kinyume cha sheria Na. 196 na 197 ya Makosa ya Jinai.

Akitoa hukumu hiyo ya kesi ya jinai ilitolewa kwa kukasimiwa madaraka (Extended Jurisdiction) na Hakimu Mkazi Mkoa wa Tabora, Jovit Kato, kutokana na ushahidi wa pande zote, ulimtia hatiani Bujije kunyongwa mpaka kufa kwa kufanya mauaji kwa kukusudia.

Alifanya kosa hilo katika Kitongoji cha Wachawaseme, kijiji cha Imagi ambako miongoni mwa mauaji yaliyofanyika kwa nyakati tofauti katika wilaya za Urambo na Kaliua mkoani Tabora.

Waliohukumiwa miaka minane jela kila mmoja kwa kutekeleza mauaji bila kukusudia yaliyotendeka katika Kitongoji cha Wachawaseme wilayani Kaliua ni Devotha Matwiga, Aman Andrew, Bosco Issa, Paulo Hassan na Peter Dundu. Wote kwa pamoja wamehukumiwa kwa kumuua Ezekia David, Juni 29, 2020.

Wengine ni Luja Clement aliyekutwa na hatia ya kumuua bila kukusudia Flora Musa Mei 9, 2020 aliyehukumiwa miaka 10 na Hosea Albert pia alihukumiwa miaka 10 baada ya kuthibitika mahakamani pasipo shaka kuwa alimuua baba yake mzazi Aprili 23, 2020.

Upande wa Jamhuri, kesi hizo zilisimamiwa na Wakili wa Serikali Veronica Moshi huku upande wa utetezi kila mtuhumiwa aliweka wakili wake kwa ajili ya kuwatetea. Kabla ya hukumu, walipotakiwa kujitetea, waliomba mahakama kuwapunguzia adhabu kwa madai kuwa wana familia, wanasomesha na wanategemewa.

Hata hivyo, mahakama haikusikiliza utetezi huo na kutoa onyo kali juu ya watu wanaojichukulia sheria mkononi na kuwataka kupitia hukumu hiyo, kuwa fundisho kwa yeyote anayejichukulia sheria mkononi bali kuwataka kufuata taratibu zote za kisheria.

# Utitiri wa michango wamchefua Katambi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Katambi, amewaagiza maofisa elimu wa shule za msingi na sekondari katika Manispaa ya Shinyanga, kufanya ufuatiliaji juu ya malalamiko kutoka kwa wazazi ya kukithiri kwa michango ya wanafunzi.

Katambi ambaye ni Mbunge wa Shinyanga Mjini, alitoa agizo hilo juzi wakati akifungua mafunzo ya utendaji kazi kwa wajumbe wa Baraza la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Shinyanga Mjini.

Alisema amekuwa akipata malalamiko mengi kutoka kwa wazazi kuwa michango ya wanafunzi imekithiri shuleni na kumwomba alifanyie kazi kutokana na kuwa kero kwao wakati serikali inatoa fedha ya kughalamikia elimu bila malipo.

"Nawaagiza maofisi elimu ngazi zote hapa Shinyanga mfuatilie haya malalamiko ya wazazi juu ya kukithiri kwa michango shuleni ili mjiridhishe na kubaini kama kweli michango ambayo wanatumwa wanafunzi kwa wazazi wao ipo kisheria kama hakuna zuieni," alisema Katambi.

Aliongeza kuwa serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia elimu bila malipo, na kuwataka walimu waache tabia ya kuchangisha wazazi michango mingi ambayo inatoa maana ya elimu bure.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Shinyanga, Grace Samweli, aliwataka viongozi wa jumuiya hiyo kila mmoja asimame kwenye nafasi yake na kujua majukumu yake ili wasiingiliane na kuleta migongano. Pia aliwataka wafanye kazi kwa kushirikiana na kuendelea kukijenga chama.

Naye Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Shinyanga Mjini, Rehema Nhamanilo, aliwasihi viongozi wote wa umoja huo, kuyazingatia mafunzo waliyopewa ambayo yatawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao ndani ya umoja huo.



Ukurasa 12

**Dk. Mwinyi sasa ni mguu kwa mguu kuanza mijadala wanaCCM kila wilaya**



Ukurasa 13

**2023 ENZI MPYA VITA AFRIKA**

Sudan rasmi ni uwanja wa mapigano wamo 'Janjaweed' Vs Jeshi la Taifa



Ukurasa 14

**WAKILI GEORGE MLAWA;**

**Asimulia alichoshuhudia gerezani wanaosubiri adhabu ya kunyongwa**


# siasa

JUMATANO MEI 10, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


MCHWA RIPOTI CAG

# Chanzo kubeza maslahi ya umma kubeba 'uzalendo wa kiubinafsi'

• Kichocheo viongozi serikali, umma kufanya biashara

Na Dk. Felician B. Kilahama

TANZANIA yaweza kuwa 'pepo ya dunia' ni kwa sababu ina kila jambo la kuvutia na kufurahisha. Zikitajwa mbuga za wanyama zipo zaidi ya 20 tena zenye mvuto wa kipekee aidha, yapo mapori ya akiba takribani 30.

Chini ya ardhi kuna aina mbalimbali za madini ukifikiria tanzanite imejaa Mererani. Kuna dhahabu, almasi, chokaa, ulanga, chuma, makaa ya mawe, bati, urani inapatikana kwa wingi pia ipo 'graphite na rubies'.

Nchi imo ndani ya maziwa makuu likiwamo Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na kumiliki ukanda wa bahari takribani kilometa zaidi ya 800. Vilevile, kuna mito mikubwa mfano, Ruaha Mkuu, Ruaha Ndogo, Kagera, Kilombero, Kihansi, Malagalasi/Moyowosi, Mara, Rufiji, Pangani, Ruvuma, Ruvu, Wami, Zigi na chemicheni nyingi nchi nzima.

Isitoshe, taifa limesheheni rasilimali misitu, nyuki kwa kiwango cha kutosha pamoja na watu ambao kulingana na matokeo ya sensa ya watu na makazi ya 2022 sasa ni zaidi ya milioni 60.

Ndani ya maji na katika wanyamapori na misitu/nyuki kuna rasilimali nyingi zenye thamani kubwa kwa taifa zikiwamo fursa nyingi za utalii na biashara.

Vitu vyote pamoja na thamani ya ardhi na mamilioni ya watu, hakika Tanzania ni taifa tajiri kuliko watu wake wanavyodhani.

Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, wakati wa uongozi wake alisema maendeleo endelevu yanahitaji vitu vinne ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Vyote kimsingi vipo, lakini ukiyatazama na kulinganisha na hatua



Moja ya nyumba za walimu katika Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa. Fedha zilizotajwa na CAG kufujwa zingetumika kuboresha miundombinu ya shule za msingi nchini, ikiwamo shule hii. **PICHA: NIPASHE**

iliyofikia kwa miaka 60 ya uhuru hupati picha kama nchi imefanya vizuri.

Miongo sita ya uhuru taifa limegubikwa na changamoto lukuki kwenye huduma karibu zote kuanzia afya, elimu, maji, kilimo, uvuvi, ufugajji, mazingira, uhifadhi, nishati, miundombinu, mawasiliano, ustawi naaendeleo ya jamii.

Kila mwenye kufuatilia anajiuliza kikwazo ni nini? Lakini, ukitupia jicho kipindi kifupi cha kuanzia 2015 hadi sasa ukiangalia yaliyofanyika unasema 'kumbe inawezekana kujikwamua' na kupunguza changamoto kikubwa ndani ya kipindi kifupi.

Pamoja na rasilimali ardhi, watu na siasa na uongozi bora, kuna udhaifu katika kusimamia matumizi ya rasilimali zilizoko ili zilete maendeleo.

Bado dhamira ya 'maisha bora kwa kila Mtanzania' inabaki kinadharia zaidi kuliko uhalisia kwa vitendo.

Tumekuwa na dira na malengo ya kifaifa kwa miaka mitano na bajeti kupitishwa na bunge ili serikali itekeleze mipangokazi ipasavyo. Pamoja na hayo yote, kumekuwepo na hali isiyoridhisha kuhusu matumizi ya fedha na vifaa ili kutekeleza malengo.

Kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali (CAG) amekuwa akitoa taarifa kuhusu utekelezaji na matumizi ya rasilimali zikiwemo fedha, nguvukazi na muda.

Muda wote 'maCAG' wanaonyesha udhaifu mwingi katika usimamizi na matumizi ya rasilimali fedha, mfano mwaka huu ripoti ya ukaguzi wa mahesabu ya serikali, ilipokabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, vyombo vya habari vilihabarisha.

Mfano ilikuwa ni taarifa:"Ripoti ya CAG nchi inatafunwa" ikifafanua kuhusu matumizi ya serikali na mashirika na kuonyesha ukiukwaji mkubwa wa taratibu na kanuni za matumizi ye fedha za umma.

Vilevile, imedhihirika kuwa hata ripoti za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), hubaini madudu mengi yanayofanywa na watendaji na watumishi serikalini na taasisi zake. Kimsingi juhudi za TAKUKURU zimekuwa zikisaidia kubaini fedha za umma zilizo hatarini kuingia mifukoni mwa 'wajanja' wachache pia kuibua kwamba ubadhirifu wa fedha na mali za Watanzania kuonekana kama ni suala la kawaida.

Kadhalika, ripoti ya CAG ya 2023 inabainisha 'madudu' katika maeneo mengi serikalini kwa kuonyesha kuwa kuna 'upigaji' wa kutisha kwenye mikataba, matumizi ya fedha zinazotolewa na serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

### VISABABISHI

Kwa ujumla visababishi vya hayo yote ni 'nafsi za kupenda kutoa na kupokea rushwa, kudorora maadili na kukosekana usimamizi na uwajibikaji wa kutosheleza. Wakati huohuo, kumekuwepo na utaratibu wa viongozi watendaji wakuu kuapa kwa utii na kuzingatia maadili.

INAENDELEA UK. 14

# Dk. Mwinyi sasa ni mguu kwa mguu kuanza mijadala wanaCCM kila wilaya



Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi akizungumza na wanachama wa katika moja ya ziara. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KWA mara ya kwanza Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar Rais Hussein Ali Mwinyi, ameanza ziara za mguu kwa mguu kuzungumza na wanachama kila wilaya. Ni baada ya kuchaguliwa kushika wadhifa huo mwishoni mwa mwaka jana. Anaahidi kuwa katika mikutano yake anataka kukijenga chama kiuchumi kwa kuimarisha miundombinu wezeshi ya utendaji kwa watendaji wake ili kupata ufanisi endelevu.

Akiwa katika ziara hiyo inayoanzia wilaya ya Magharib B, Unguja, anasema ili chama kifanye kazi kwa ufanisi ni lazima kiwe na vifaa vikiwemo vyombo vya usafiri na vya ofisini tena vya kisasa vyenye hadhi inayolingana na umri wa chama hicho, akiahidi:"Tutafanya kila linalowezekana kukijenga chama kiuchumi."

Aidha, Dk. Mwinyi anaahidi kutendea CCM makubwa zaidi wakati huu wa uongozi wake ikiwemo kujenga ukumbi mkubwa wa kisasa wa mikutano ambao chama kitajivunia kuwa na kitu bora kwa nchi nzima na kusisitiza kuwa maendeleo makubwa yaliyofikiwa Zanzibar ni utekelezaji wa ilani ya chama ambayo kwasasa imefikia nusu ya utekelezaji wa ahadi zake na kwamba sehemu ndogo iliyobaki itakamilishwa kwa wakati.

Anakumbusha kuwa CCM ina rasilimali nyingi ambazo baadhi bado hazijatendewa haki na kutumiwa kuleta maendeleo ya chama na taifa na hilo atalifanyia kazi kwa ajili ya kuwa na chama imara kinachojitegemea.

> Wakati wa chaguzi zote huibuka makundi mbalimbali yenye dhamira na maslahi tofauti hivyo, ni wakati wa wanaCCM kurejesha umoja na mshikamano mara baada ya uchaguzi kukamilika.

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Mwinyi, anaagiza chama kuwapa mafunzo ya uongozi watendaji wa ngazi zote walioshinda kwenye uchaguzi uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana pamoja na kujipanga tena kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Anaweka bayana dhamira ya kuzihuisha mali zinazomilikiwa na CCM kwa lengo la kukiendeleza chama hicho akieleza kwenye ziara yake hiyo ya kutembelea majimbo mbalimbali ya chama, anaangalia fursa zilizopo sehemu hizo na kuona jinsi ya kuwekeza kibiashara ili kukiinua chama kiuchumi.

Makamu Mwenyekiti Mwinyo, anaeleza kuwa ndani ya kipindi kifupi cha uongozi wake, anatarajia kukiona chama kinawekeza kwa vitendo miradi mbalimbali ya uwekezaji ili ikiimarishe na kuleta mabadiliko.

Pia, anawataka wanachama wa CCM kuiendeleza miradi iliyopo wakati mingine inayotarajiwa kuanza hivi karibuni kwa nia ya kuimarisha nguvu chama kimkakati na uchumi pamoja na kuziboresha ofisi za chama hicho kuendelea kuwa na hadhi ya Chama.

### AONYA MAKUNDI

Akizungumzia suala la umoja na mshikamo ndani ya chama hicho, Makamu Mwenyekiti huyo, anaonya mafarakano na mgawanyiko ndani ya CCM na kuwaasa wanachama wawe kitu kimoja ili kuongeza nguvu ya chama chao.

Anasema wakati wa chaguzi zote huibuka makundi mbalimbali yenye dhamira na maslahi tofauti hivyo, ni wakati wa wanaCCM kurejesha umoja na mshikamano mara baada ya uchaguzi kukamilika.

Aidha, anaonya endapo ikitokea hali ya mgawanyiko wa makundi ndani ya chama hicho, ameziagiza kamati za maadili kuchukua hatua kali za nidhamu na kuhakikisha nidhamu na mshikamano ndani ya chama unarejea.

Akizungumzia suala la uhai wa chama, Makamu Mwenyekiti, anawataka viongozi wenye dhamana kwa mujibu wa nafasi zao ndani ya chama hicho, kutekekeza jukumu na kuongeza wanachama wepya ili kuendelea kukipa uhai chama hicho kiendelea kushika dola.

"Mtaji wa chama chetu ni kuongezeka wanachama wepya, kadi ziwepo za kutosha" anasisitiza Makamu Mwenyekiti na kuhimiza wana CCM kulipa michango kwa wakati badala ya kusubiri hadi vipindi vya uchaguzi vikaribie.

Naibu Katibu Mkuu CCM, Zanzibar Dk. Muhamed Said Dimwa, anasema CCM haitajibu maneno wanayorushiwa na wapinzani badala yake wataendelea kuitekeleza ilani ya chama chao kwa kuboresha maendeleo ya nchi na watu wake na kuahidi kutowafumbia macho wenye dhamira ya kukwamisha ilani ya chama hicho.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa, na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, anawaasa wanachama CCM kuwachagua viongozi wenye sifa na weledi wa kuwatumikia wananchi na sio kuwanunua viongozi wakati wa chaguzi za chama hicho.

Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Zainab Khamis Shomari, anaeleza ahadi ya wanawake Tanzania bado ipo palepale ya kurejesha ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi mkuu wa 2025, aidha anaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwajengea heshima wanawake kwa kuwapa fursa ya uongozi kwenye sekta mbalimbali.

Akizungmza kwa nyakati tofauti wakati akiorodhesha mali za chama hicho, Katibu wa Kamati Maalum NEC, Idara ya Uchumi na Fedha kutoka ofisi Kuu ya cha CCM Kisiwandui, Afadhali Taibu Afadhali, anayataja maeneo ya kimkakati yanayomilikiwa na chama hicho ikiwamo eneo latawi la CCM Mbweni, ukumbi wa CCM Maisara, nyumba ya kumbukumbu ya Afro - Shiraz iliyopo Posta ya Kijangwani pamoja na kituo cha mafuta Kinazini.

Baadhi ya wanachama wa chama hicho, wanaeleza kufurahishwa na hatua ya kiongozi huyo katika kukijenga chama kiuchumi kwa kuimarisha miundombinu wezeshi ya utendaji kwa watendaji wake ili kuboresha ufanisi ndani yaCCM.

2023 ENZI MPYA VITA AFRIKA

# Sudan rasmi ni uwanja wa mapigano wamo 'Janjaweed' Vs Jeshi la Taifa

• Majenerali wawili wakabana koo kugombea madaraka

**Na Ani Jozeni**

JITIHADA za kuikwamua Sudan katika janga la vita zinaendelea washirika wakiwamo Saudia Arabia wanakutana na majeshi yote mawili la serikali na la Rapid Support Forces (RSF) au 'Janjaweed' kutafuta usuluhishi.

Hivi karibuni, Sudan Kusini ambayo ni mtoto wa Sudan inayopigana, imewakutanisha wakuu wa pande mbili za jeshi la nchi hiyo zilizo vitani.

Kuacha mapigano bado ni mfupa mgumu kwani pande mbili za jeshi zinajitahidi kukamata maeneo na kujipanga kikamilifu kuendelea na mapambano, au kufanya majadiliano katika hali ya usawa kwenye uwanja wa vita. Zaidi ni vikosi maalum (Rapid Support Forces) vinavyohitaji kujiimarisha, kwani jeshi la nchi lina uhalali wa kisiasa wakati vikosi hivyo vipo na havitishiki.

Wakati hakuna dhamira ya kuelekea katika muafaka wa aina yoyote kwani hitaji la kujipanga katika uwanja wa vita bado ndilo linalotawala katika suala hilo. Kimsingi jeshi linataka utawala wa kiraia ukubaliwe, na siyo kuwapiga waandamanaji kila uchao, kuvuruga amani ya nchi na kuyaachia makundi ya maharamia (likiwamo jeshi la ziada la vikosi vya RSF kuingia katika biashara ya dhahabu na kuiuza kwa maslahi yao. Likiamini kuwa mparaganyiko huo hulea uharamia.

Msuguano kati ya Jeshi la Sudan na vikosi maalum unaanzia miaka zaidi ya wiki kadhaa sasa ambako sera za ukandamizaji za Rais Omari el-Bashir kuruhusu tabaka la mamwinyi wanaohitaji ardhi ya kupanua maeneo ya mifugo kutenda watakavyo hasa eneo la Darfur, magharibi ya nchi hiyo.

Kadhia hiyo ilikuwa ya maeneo mengi ila kwa sababu za kiuchumi (kulengwa zaidi eneo hilo na makundi ya Janjaweed au askari wanaokimbia au kuchanja-mbuga wakipanda ngamia kuenea kote, eneo hilo lilifahamika zaidi. Ikabidi utawala wa kijeshi wa Sudan ukubali vikosi vya Umoja wa Mataifa (UN) vilinde amani, ikwepe vikwazo au hata kushtakiwa kwa mauaji ya watu wengi ya kudhamiria.

Hali hiyo iliingia katika hatua nyingine wakati wa mapinduzi nchi za Kiarabu mwaka wa 2011 ambako tawala kadhaa ziliangukа, hivyo Sudan nayo ikaingia katika mvutano. Ule uhusiano mtulivu kiasi kati ya jeshi, makundi ya kiraia tabaka la mamwinyi, uelekeo wao wa kutaka sheria (yaani utawala wa jadi wa viongozi wa kidini na siyo sheria za nchi zinazosikilizwa mahakamani zilizoachwa na utawala wa Uingereza, mwaka 1956), ukaanza kuingia mashakani.

Tabaka la mamwinyi linataka utawala mkali wa kijeshi, na siyo 'weledi' wa jeshi la Sudan kuafikiana na Kamati ya Madaktari wa Sudan ili kuelekea katika serikali halisi ya mpito, ilivyotangazwa na Jenerali al-Burhan akiwa anaona ulazima wa Sudan kutengemaa, kuwa hali ya kawaida.



Mohamed Hamadan Dagolo, kamanda wa zamani wa Janjaweed, anayebeba hatima ya Sudan akiviongoza vikosi vya RSF vinavyoazimia kutwaa uongozi. **PICHA ZOTE: REUTERS**



Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, kiongozi wa kijeshi wa Sudan, ambaye ni rais na mkuu wa majeshi, anayetishiwa na RSF.

**JESHI LAZIDIWA**

Kwa maana hiyo RSF ni tegemeo la tabaka la mamwinyi, ila hawajisifii kwa umwinyi na hujitambulisha kwa uwazi zaidi kama maimamu. Ukiangalia hali ya uwanja wa mapambano unapata picha kuwa jeshi ni kama limezidiwa na hali ilivyokuwa inaenda jeshi lilikuwa linazidi kusukumwa pembani.

RSF ina nguvu katika sehemu kubwa zaidi ya jiji la Khartoum mji mkuu, ila kwa maeneo kadhaa kama ikulu na nchi hiyo, kambi kuu ya kijeshi, radio na televisheni za serikali na karibuni RSP iliteka gereza kuu la Khartoum na kufungulia wafungwa na mara kadhaa wanaonekana kuzingira ikulu anakokaa al-Burhan.

Miongoni mwa nchi za Ghuba ikiwamo Saudia inaelekea wameweka msimamo wa kuitaka RSP ichukua madaraka, kiasi kwamba kulikuwa hata na mahojiano maalum ya kushangaza katika televisheni ya Al Jazeera inayomilikiwa na Qatar, rafiki wa Iran. Ilikuwa ni kuonyesha wazi kumtakia Meja Jenerali Mohamad Hamdan Hemedti 'Dagalo 'mkuu wa RSF na mtesaji mkuu wa Darfur miaka iliyopita.

Nchi hizo zinamtegemea apeleke dhahabu ya Sudan kwao kwa bei poa, na siyo irudi hali ya kawaida maeneo hayo yatolewe kwa wawekezaji kutoka nchi za Magharibi. Isitoshe wana uhusiano wa karibu na matabaka ya jadi ya Sudan, kwani kama wasemavyo Waswahili, 'Waarabu wa Pemba hujuana kwa vilemba.'

Siyo rahisi kusema upepo wa vita unaelekea upande gani hasa, kwani wenye uchu zaidi wa vita ni RSF na hakuna uhakika kuwa Jeshi la Sudan kwa jumla liko nyuma ya Al-Burhan kutaka kurudisha utawala wa mpito kuelekea uchaguzi halisi. Ila RSP na wenzao wa Ghuba hawana uwezo wa kukabiliana na janga la kibinadamu linalotokana na pande hizo mbili za majeshi ya Sudan kuingia rasmi vitani.

Si rahisi kusema ni sehemu gani ya watu wa Sudan ambao haihitaji chakula cha msaada kutoka nje, wakati zaidi ya nusu, au theluthi mbili, za hospitali za Khartoum zimefungwa, kuashiria kuwa taabu za wananchi wa Sudan zinafikia kilele cha kutisha, kuogofya na hata kutishia maisha.

Ziko nchi kama Syria, Libya au Yemen zimekuwa katika vita vya aina hiyo, majeshi yanayolingana nguvu yakipambana kuidhibiti nchi. Tofauti ni kuwa walikuwa wanapigania nje ya mji mkuu au kwa upande mwingine mji mkuu unakuwa na uwezo wa kumudu hali ya kawaida kwa kiasi fulani.

> Licha ya kuwa Sudan ina mali ambazo Yemen haina, na tabaka tawala (kijamii) limepania kuidhibiti nchi kwa kutumia RSF, haitakuwa rahisi kwa jeshi la Sudan kujisalimisha kwa vikosi hivyo.

Kwa msingi huo walioko madarakani wanawaaminisha watu kuwa inawezekana kufaulu, hivyo waendelee kujitahidi na kama ni wanaotaka kuteka nchi, hawaaibiki sana kwa janga la kibinadamu linalotokana na vita hivyo kama ilivyokuwa Yemen.

Imefikia mahali hivi karibuni China ikazikutanisha Iran na Saudia, ila si rahisi kusema nani alitoa wazo hilo na kukubalika. Inawezekana ni Iran, kupanua wigo wa kukubalika katika eneo hilo, kwani janga la kibinadamu la Yemen, hasa vifo vya watoto wadogo kwa kukosa chakula, lishe na dawa, lilifikia ngazi ya kutisha, kuusuta mpangilio mzima wa kiitikadi wa mgogoro huo.

Licha ya kuwa Sudan ina mali ambazo Yemen haina, na tabaka tawala (kijamii) limepania kuidhibiti nchi kwa kutumia RSF, haitakuwa rahisi kwa jeshi la Sudan kujisalimisha kwa vikosi hivyo na nchi iingie kwenye utawala wa kiimla na kijadi.

Na kabla haijafikia hapo, upo uwezekano wa RSF kukosa msingi wa kijamii kuendesha mapigano, endapo hata tabaka la mamwinyi linapokuwa mashakani nchi nzima ikiwa taabani, wanaendelea kujazana mipakani na waliobaki hawajui waishije, nchi haina dawa, maji, umeme wala uongozi.

JUKWAA LA VIONGOZI

WAKILI GEORGE MLAWA;

# Asimulia alichoshuhudia gerezani wanaosubiri adhabu ya kunyongwa

**Na Christina Mwakangale**

DUNIANI kila binadamu anafahamu kuwa iko siku ataondoka au kufa, japo hajui lini kifo kitatokea na kuagana na hii dunia ambayo wengi wanaipenda na wasingetamani kusikia kuwa kuna wakati wataiacha.

Ukiwaangalia waliohukumiwa adhabu ya kifo, wakitamkiwa na hakimu kuwa watanyongwa hadi kufa, miongoni mwao wengi hupata msongo wa mawazo na kufadhaiki wakati wa kusubiri kuuawa au kunyongwa wakiwa magerezani kama ambavyo maelekezo ya mahakama au hukumu yalivyoagiza.

George Mlawa, wakili, aliyewahi kuwa Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, lakini na Katibu wa Bunge, anasema ametembelea baadhi ya magereza yenye wafungwa walitamkiwa kuwa watanyongwa hadi kufa na kueleza kuwa wahusika hao hupitia wakati mgumu mno kwenye maisha yao.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na gazeti hili jijini Dar es Salaam, baada ya kutoa maoni kwenye Tume ya Kuangalia Namna ya Kuboresha Mifumo ya Haki Jinai, iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, anasema waliohukumiwa kufa kuna baadhi wamepoteza fahamu baada ya hukumu hiyo na wengi wao wakifika gerezani huwa watu wema, wakiabudu tena muda mwingi wakisoma Biblia na Quran.

Anatoa maoni katika tume hiyo inayoongozwa na Mwenyekiti Jaji Mkuu Mstaafu, Othman Chande na Makamu Mwenyekiti ni Balozi Ombeni Sefue; wajumbe wengine ni pamoja Jaji Dk. Eliezer Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Prof. Edward Hosea; Said Mwema; Balozi Ernest Magu; Dk. Laurean Ndumbaro na Omary Issa.

"Adhabu ya kunyongwa mpaka kufa. Hilo neno mpaka kufa linaainisha, hata mnyongwaji aponyoke, adhabu ni kunyongwa mpaka afe, tamko hilo linasababisha wengine kupoteza fahamu. Ilikuwa ni kitu cha kuhitaji moyo na kuwa na moyo mgumu," anasema na kuongeza kuwa alitembelea baadhi ya magereza mwaka 2009.

"Nilitembelea Gereza la Ruanda Mbeya huko niliwakuta pale watu ambao wamehukumiwa kunyongwa na walikuwa zaidi ya 20 na walikuwa hawajanyongwa," anakumbusha Mlawa, ambaye amekuwa Katibu wa Bunge.

Kwenye mahojiano na baadhi yao, anasema walimpa simulizi tofauti na kuongeza kuwa walikaa eneo lao maalumu na wakamwambia kuwa wengine wamekaa zaidi ya miaka 10 hawajanyongwa. Hakuna kitu kinachoumiza na kilichowaumiza wanasema zaidi ya kusubiri kifo.

"Mara nyingi unakuja kujua kuwa unatakiwa kunyongwa usiku wa kuamkia siku yenyewe ya kunyongwa, labda alfajiri saa 10 na anakuja ofisa wa magereza, kukwambia saa moja asubuhi utanyongwa. Kama ni Muislamu au Mkristo anaitwa mtu maalumu kwa ajili ya kufanya sala saa chache na kweli saa moja kamili asubuhi mfungwa unanyongwa," anasimulia.

Anasema kwenye kipindi cha awamu ya tatu cha Rais Benjamin Mkapa hakunyongwa mfungwa, Mkapa alikuwa hataki kusaini vifo na pia hakusaini watu kunyongwa kwa miaka yote ya uongozi wake, rais katika utawala wake anaweza kusaini kunyongwa au kutokunyongwa na badala yake kikiwa kifungo cha maisha," anasema.

"Walisema magereza haijapewa ruhusa na rais ndiyo maana wako wengi gerezani kutokana na hilo, wote waliokuwa majambazi wamekuwa wacha Mungu sana kutokana na kuhofia kunyongwa muda wowote. "Hiyo tuliona ni mateso kwa hiyo mimi nilivyorudi na wengine waliokwenda kutembelea magereza mengine na kuonana na wafungwa waliohukumiwa kunyongwa nikatoa taarifa hiyo kwa hakimu," anasema Mlawa.



Aliyewahi kuwa Katibu wa Bunge, Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, George Mlawa. **PICHA: MTANDAO**

Anasema wakati huo, hukumu hiyo ilipingwa duniani na badala yake ikashauriwa adhabu iwe kifungo cha maisha. "Presha' kwa nchi zingine ilikuwa ni kupunguza adhabu ya kifo na badala yake waweke kifungo kama cha maisha jela.

**ADHABU KIFO IBAKI**

Ana maoni kwamba adhabu ya kifo isifutwe ingawa utekelezaji wake unaweza usifanyike, ili kuweka fundisho kwa watenda makosa yenye kuhitaji adhabu hiyo na kuongeza kuwa unahitajika uchunguzi, ili taifa lipate maoni ya wananchi kujua wanasemaje na alipata ya mkoa wa Mbeya na wenzake wakaenda magereza mengine wakaona kunyongwa sio ustaarabu.

"Tulikutana na mapokeo ya kupinga kufuta adhabu ya kifo, wananchi wakatuambia watu wa serikali sio nyie mnaouawa bali ni sisi ninyi mmekaa huko katika ustaarabu wenu ...Sisi tunaonekana hamtujali na tutafanya basi lolote kama sisi," anasema kauli za watoa maoni ziliporejeshwa tume hiyo, zikitoka mikoa tofauti ziliwaweka njiapanda, iwapo adhabu ifutwe au ibaki.

**UONGOZI SERIKALINI**

Anasema kwa uzoefu wake, akiwa Mwanasheria wa Serikali kwa miaka mingi, akiendesha kesi za mauaji na nyingine na wale waliohukumiwa na kutiwa hatiani, alikuwa kama mshauri wa serikali. Amepitia chuo ni kuhusu ushauri wa kisheria na hilo lilimfanya awe imara, kisha amekaa miaka mitano huko chuoni akipata ujuzi huo na baadaye Rais Ali Hassan Mwinyi, alivyopendekeza tume ya katiba ya mfumo wa vyama vingi iliyoongozwa na Jaji Nyalali, akiwa kiongozi wa washauri na kwamba baada ya hapo, aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge na mshauri wa Spika.

"Nilipata nafasi ya kujifunza mitaala ya mabunge yenye vyama vingi duniani kama Canada, Marekani, India na Australia na mwaka 1995 likaanza bunge la vyama vingi na nimekuwa, Katibu wa Bunge mpaka mwaka 2000 kwa muda wa miaka tisa na hakuna aliyekaa kwa muda mrefu kama huo." Anasema.

Anasema baadaye akawa mbunge wa Kalenga, Iringa na baadaye akaja kuwa Kamishna wa Tume ya Haki na Utawala Bora na kule ndiko alipokwenda kupata mambo na kuja kutoa maoni yake kwenye Tume ya Kuangalia namna ya Kuboresha Mifumo ya Haki Jinai.

## Chanzo kubeza maslahi ya umma kubeba 'uzalendo wa kiubinafsi'

**INATOKA UK. 11**

Swali linakuja kwamba inakuwaje walioapa wanapochukua madaraka au kutekeleza majukumu wahusike katika ubadhirifu na kuwasimamia ipasavyo waliochini yao? Kimsingi, kinachosababisha hayo yote ni maslahi binafsi ndicho chanzo cha kudhoofisha shughuli za umma na kuendelea na uduni kimaendeleo.

Kabla ya 'kufuta' kanuni ya kuwazuia viongozi au watendaji wakuu serikalini pamoja na mashirika na taasisi zake, walikuwa hawaruhusiwi, kwa manma yeyote ile, kujihusisha na shughuli zozote za biashara.

Yeye aliye madarakani pamoja na jamaa zake, kanuni hiyo ililenga kuhakikisha watunga sera au wafanya maamuzi wanasimamia shughuli za serikali na kufanya maamuzi sahihi bila upendeleo wa aina yoyote.

Lakini baada ya kuiondoa kanuni hiyo, kila mtu akawa huru kufanya au kujihusisha na shughuli za biashara. Hapa ndipo maslahi binafsi yaliposhamiri na kuzitawala nafsi za wengi wenye madaraka.

Mathalani, tunaangalia masuala mawili muhimu umma na sekta binafsi, wafanya biashara pengine wawekezaji. Wanasiasa watunga sera, wasimamizi utekelezaji sheria hususani wanaofanya maamuzi nini kifanyike au kisifanyike maslahi binafsi yatazingatiwa.

Wanapofunguliwa 'mlango' wa kushiriki katika shughuli za kibiashara imekuwa changamoto kubwa hasa kwa mataifa yanayoinukia kiuchumi kama Tanzania.

Kwa hiyo nchi imepoteza dira au dhamira thabiti ya 'kuujenga umoja wa kitaifa' maana kunakuwepo na fursa ya mhusika serikalini kufanya maamuzi yatakayolenga yeye anufaike zaidi kuliko taifa kwa kuwa ubinafsi unakumbatiwa zaidi.

Hata kama tunapitisha mipango kwa madhumini ya kujenga taifa letu wakati huohuo, watekelezaji wa mipango husika ndiyo haohao wenye 'mikono yao' katika biashara tusitarajie miujiza.

Watafanya maamuzi yatayoegemea zaidi 'maslahi binafsi' kuliko umma, na kuzidi kuchangia kukosekana kwa maisha bora kwa kila Mtanzania.

Tukichunguza kwa undani tunaweza kuona kwamba ubadhilifu serikalini haufanyi mtu mmoja pekee. Kunakuwepo na 'mnyororo wa aina yake kuwezesha watu kadhaa kunufaika.

Waliomo kwenye sekta ya umma na binafsi pia hawa ndiyo TAKUKURU inawaita 'wajanja' wa kuchepua fedha za kutekeleza shughuli za umma, zikaingia mifukoni mwao.

Mathalani, kufanya mashine za kielekroni za kukusanya mapato badala ya kuingiza fedha katika akaunti sahihi, zinaingia kwenye akaunti binafsi na inakuwa vigumu kugundua haraka maana pia usimamizi unakuwa unalegalega (kwa kuwepo mianya ya kujinufaisha).

Nilibahatika kutembelea karibu mikoa na wilaya zote nchini wakati wa utumishi serikalini. Mwaka 2010 nilitembelea wilaya kadhaa lakini nilifika mkoa mmoja nikakuta wilaya ambayo ofisi ya Mkuu wa Wilaya inapendeza kutokana na ukaratabi uliokuwa umefanyika. Hivyo, nilitaka kujua imekuwaje ofisi yake inang'ara wakati sehemu nyingi nilizopita Ofisi za Wakuu wa Wilaya zilikuwa hazitamatiki kwa kutofanyiwa matengezezo ya muda mrefu.

Alicheka kidogo, lakini akajibu kwamba ameamua aifanyie matengezo kwa kutumia kiasi kidogo cha fedha anazopata kutoka serikali kuu lakini hakupenda kuzungumzia suala hilo zaidi ya hapo.



# Serikali yatangaza ajira milioni 3 katika kilimo

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amesema wizara yake inatarajia kutengeneza ajira mpya milioni tatu kwa wanawake na vijana ifikapo mwaka 2030.

Pia inatarajia kuongeza thamani ya mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka dola za Marekani bilioni 1.388 (Sh.trilioni 3.2) mwaka 2023 hadi hadi Dola za Marekani bilioni 1.457(Sh. trilioni 3.4) mwaka 2023/2024.

Alitaja mikakati hiyo juzi bungeni mkoani Dodoma wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara yake, huku akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 970 ili kutekeleza mikakati na vipaumbele ilivyopanga.

Bashe alisema mpango na bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2023/2024 umelenga kujenga sekta ya kilimo endelevu itakayowapa fursa vijana na wanawake kushiriki kwenye kilimo biashara.

Alisema lengo ni kutoa fursa za ajira zenye staha na kipato cha uhakika ili kufikia lengo la ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 na kuondoa watu kwenye umasikini.

Bashe alisema maeneo makubwa ya uwekezaji ni ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, miundombinu ya uhifadhi, uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoja, upatikanaji wa pembejeo, utafiti na huduma za ugani.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo utaimarisha usalama wa chakula wakati wote na kukuza uchumi shirikishi ambao utaboresha maisha ya mkulima na kuleta utajiri kwa taifa.

Bashe alisma uwekezaji huo utachangia upatikanaji wa ajira kwa vijana na wanawake kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 ambayo imeelekeza kutengeneza ajira milioni nane kwenye sekta zote

# Kinamama 142, watoto 1,968 wafariki Singida miaka mitatu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANAWAKE 142 na watoto wachanga 1968 wamefariki dunia mkoani Singida katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2020 kutokana na matatizo ya uzazi.

**Mwaka 2021 vifo 44 kwa kinamama na 681 kwa watoto na mwaka 2022 vifo 52 kwa kinamama na 540 kwa watoto wachanga.**

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Victorina Ludovick, alibainisha hayo juzi alipofunga kikao kazi kilichofanyika Halmashauri ya Itigi cha kujadili vifo vya kinamama na watoto vitokanavyo na uzazi kwa lengo la kupanga mikakati ya kupunguza vifo hivyo.

Dk. Ludovick alitoa mchanganuo kuwa mwaka 2020 vilitokea vifo 46 vya kinamama na 747 vya watoto wachanga. Mwaka 2021 vifo 44 kwa kinamama na 681 kwa watoto na mwaka 2022 vifo 52 kwa kinamama na 540 kwa watoto wachanga.

Alisema kuongezeka kwa vifo hivyo kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wazazi kutohudhuria kliniki au kituo cha kutolea huduma kwa wakati.

Dk. Ludovick alisema sababu nyingine ni ubovu wa miundombinu ya barabara katika maeneo mengi, hasa ya vijijini, uhaba wa dawa na vifaa katika vituo vya kutolea huduma na watoa huduma kushindwa kufanya uamuzi sahihi wa kutoa rufani kwa wakati.

Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Singida, Hyasinta Alute, alishauri jamii ielimishwe kuhusu umuhimu wa kinamama kuanza kliniki mapema ili wapate huduma muhimu kwa wakati na kuongeza kuwa idara ya afya mkoa imeendelea kushirikiana vizuri na mfumo wa M-MAMA ili kuokoa vifo vya kinamama na watoto wachanga.

Kiongozi wa Timu ya Huduma Mkoba kutoka Shirika la Marrie Stopes, Flora Shirima, alisema yapo maeneo yanahitaji kupewa kipaumbele na kuahidi kufanyia kazi ombi la kusaidia timu ya dharura ili kuokoa maisha ya makundi hayo mawili.

Meneja wa Damu Salama Kanda ya Kati, Dk. Kitura Mthias, alisema Mkoa wa Singida umefanya vizuri katika ukusanyaji wa damu kwa asilimia 135.87.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akiongoza kikao cha kamati ya uongozi kilichopitia ratiba ya mkutano wa kumi na moja wa Bunge unaoendelea jijini Dodoma jana na kuongeza muda wa vikao kwa wizara zenye wachangiaji wengi. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# TAWA yaandaa mpango shirikishi miaka 3 Pori la Akiba Kilombero

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imeandaa mpango shirikishi wa miaka mitatu (2023 - 2025) wa usimamizi wa Pori la Akiba Kilombero.

Akiuwasilisha jana kwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Kamishna wa Uhifadhi wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joas Makwati, alisema mpango huo unalenga kufanikisha masuala ya ulinzi, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali ya maji na wanyamapori.

Alisema pori hilo lina umuhimu mkubwa kwa taifa kutokana na kuchangia asilimia 65 ya maji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo linatarajia kuzalisha MW 2,115 za umeme.

"Pori hili ni chachu ya kufungua fursa za utalii ikiwamo shughuli za uwindaji wa kitalii ambazo zinaongeza fedha nyingi za kigeni, ikizingatiwa kuwa mpaka sasa pori hilo lina vitalu vinne vya uwindaji wa kitalii," alisema.

Makwati alisema katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2020/21, TAWA ilitoa Sh. milioni 425 kwa Halmashauri za Wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi kama gawio la asilimia 25 ya mapato yatokanayo na shughuli za utalii katika pori hilo.

Makwati alisema TAWA imetoa fursa kwa wananchi kufanya shughuli za uvuvi kwa utaratibu maalum katika pori hilo, jambo ambalo limewanufaisha wakazi wa Kilombero.

Pamoja na hayo, alisema TAWA imeboresha miundombinu kwa kuweka alama za mpaka, vigingi 301 kati ya 1,686 vimewekwa, ujenzi wa kambi mbili za doria, kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi 9,861 wa vijiji 16 katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Anderson Mutatebwa, alifafanua suala la kisera kuhusu tathmini inayofanywa na serikali kwa wananchi wa Kijiji cha Ngombo na vitongoji vilivyopendekezwa kuondolewa nje ya hifadhi.

Mwenyekiti wa kikao hicho cha kamati, Augustino Vuma, alipongeza TAWA, akisema kamati inatambua jitihada zao katika kulinda mazingira na rasilimali zilizopo ndani ya hifadhi hiyo kwa manufaa ya taifa.

# Wanaotupa taka katika mifereji sasa kukamatwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Mazingira wa Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro amewaagiza watendaji wa kata na mitaa kuwakamata watu wanaotupa taka katika mifereji ya maji.

Akizungumza juzi na wakazi wa Kata za Miyuji na Mnadani jijini hapa baada ya kufanya usafi wa mazingira, Kimaro alisema watendaji hao wanapaswa kutekeleza wajibu wao kwa kuwakamata wanaochafua na kuharibu mazingira ya mifereji ya maji taka.

Alisema usafi unatakiwa kuwa sehemu ya tabia ya mtu, hivyo uanzie majumbani kwa kufanya usafi na kutunza mazingira.

"Hivyo, wale wote ambao hawafanyi usafi na kuchafua mazingira kwa makusudi wasionewe aibu, bali wakamatwe na kupewa adhabu kwa mujibu wa shera bila kuonewa huruma,"aliagiza.

"Ufanyaji wa usafi wa uhakika unapunguza magonjwa kwa asilimia 75,yakiwamo ya milipuko kama vile kipindupindu ambayo huigharimu serikali mabilioni ya shilingi pindi yanapojitokeza," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Karume, Matwiga Kyatya, aliwahimiza wananchi wa kata hiyo kuimarisha ulinzi na usalama kwenye maeneo yao na kuwataja bila kuwaonea aibu wanaojihusisha na wanaonekana kuwa tishio kwa amani na usalama katika kata hiyo.





# Mwalimu, mlinzi kizimbani kesi ya kujeruhi mwanafunzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Rohila, Kata ya Utengule Usongwe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Emmanuel Kamili (29), na mlinzi wa shule hiyo, Haruni Kerupe (30), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka ya kumpiga na kumjeruhi mwanafunzi.

Akisoma hati ya mashtaka jana mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya, Paul Ntumo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Emelda Aluko alidai washtakiwa walitenda kosa hilo Februari 12 mwaka huu.

Alidai kuwa siku ya tukio, Mwalimu Kamili na Mlinzi Kerupe, wote wakazi wa Lwala mjini Mbalizi, walishirikiana kumpiga mwanafunzi wa kidato cha nne, Laurance Mwangake, wakimtuhumu kudokoa maandazi katika duka la shule.

Alidai kuwa kipigo hicho kilimsababishia maumivu makali na kitendo hicho ni kinyume cha kifungu namba 225 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16.

Mshtakiwa wa kwanza, Kamili alikana kutenda kosa hilo, lakini akakiri kumkaba mwanafunzi huo huku mshtakiwa wa pili, Kerupe, akiwakilishwa mdhamini wake. Mshtakiwa huyo hakuwapo mahakamani.

Mwendesha Mashtaka, Emelda Aluko, alidai upelelezi wa shauri hilo umekamilika, akiahidi kuwasilisha ushahidi mahakamani ili kuthibitisha tuhuma dhidi ya wawili hao kumpiga na kumjeruhi mwanafunzi huyo.

Hakimu Mkazi Mkuu Ntumo aliahirisha kesi hiyo kwa ajili ya uchambuzi hoja za awali kisha kuanza kusikiliza shauri hilo la jinai. Mshtakiwa wa kwanza aliachiwa kwa dhamana.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati), akionyesha namna wadau wa elimu wanavyoweza kuchangia kwa simu ujenzi wa hosteli za wanafunzi wa kike katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya, ili kuwasaidia kusoma kwa utulivu. Kulia ni Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. William Mwegoha na Mkuu wa Ndaki ya Mbeya, Prof. Henry Molel. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# DC aagiza upandaji wa miti kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya amewataka wakazi wa Jiji la Mbeya kupanda miti kwa wingi ili kufyonza hewa ukaa na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Beno Malisa pia amesema miti hiyo baadaye wataiuza na kupata fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo, ikiwamo kuendeleza miundombinu ya elimu na barabara za jiji hilo.

Alitoa rai hiyo juzi alipozindua upandaji miti ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya, akisema "...tunapanda miti ili kuhakikisha tunatunza mazingira. Miti hii ni biashara kubwa ya hewa ya ukaa.

"Tunazo halmashauri ambazo zinavuna kiwango kikubwa cha fedha na kuwekeza kwenye elimu na barabara kwa kuvuna hewa ya ukaa kutokana na miti iliyooteshwa. Hivyo, lazima na sisi Mbeya tuige huo mfano kwa maana ya faida zote mbili." Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Mganga Mkuu wa Jiji la Mbeya, Dk. Jonas Lulandala alisema wamejipanga kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo na tayari wamefanya uhamasishaji kwa watumishi na wananchi wengine ili kufanikisha mkakati huo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Magufuli, Obadia Kabuje alisema shule hiyo imekuwa na jitihada za kupanda miti ya matunda na kivuli kwa lengo la kutunza mazingira na wanatarajia kuendelea kuelimisha wanafunzi ili kujenga uelewa kuhusu umuhimu wa upandaji miti kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Baadhi ya wadau wa mazingira katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya walisema ili kufanikisha upandaji miti, lazima kuwapo na ushirikiano baina ya serikali, wananchi na sekta mbalimbali ili kila mmoja atimize wajibu wake.

## TCRA yawataka wasafirishaji wa vipeto, vifurushi kusajiliwa rasmi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MENEJA wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Asajile John, amewataka wasafirishaji wote wa vifurushi na vipeto wanaofanya kazi katika kanda hiyo, kurasimisha huduma zao za usafirishaji kwa kuchukua leseni kutoka mamlaka hiyo.

Akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa huduma za posta jana mjini hapa, Asajile alisema umiliki wa leseni ya TCRA unaongeza mapato kwa watoa huduma kwa kuwa wateja wengi wanavutiwa zaidi kutuma mzigo kwa watoa huduma walio rasmi.

Alisema kuongezeka kwa wateja pia kunaongeza mapato ya watoa huduma na hivyo eneo hilo kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

Asajile aliongeza kuwa ili kufanikisha hilo, TCRA imeanzisha mfumo wa utoaji leseni mtandaoni ilioupa jina la Tanzanite, ambao mtoa huduma anaweza kuomba kupata leseni kwa njia ya mtandao, jambo ambalo linarahisisha utendaji na kuepusha gharama.

Alisema kuwa iwapo waombaji hao wa leseni wakikumbana na vikwazo katika kuomba leseni, wawasiliane na TCRA kupitia namba ya dawati la huduma ambayo ni 0800008272 au kufika katika ofisi yoyote ya mamlaka kwa msaada zaidi.

Mkutano huo ni sehemu ya kampeni ya kuhamasisha wananchi kutumia huduma za watoa huduma wa kusafirisha vifurushi waliosajiliwa.

## Waitaka serikali kukarabati miundombinu Chuo cha Afya

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WANAFUNZI na walimu wa Chuo cha Afya Songea, wameiomba serikali kufanya ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Songea kwa kuwa sasa iko katika hali mbaya ya uchakavu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho walioomba hifadhi ya majina, walisema majengo ya chuo yako katika hali mbaya. Yamechakaa. Hayajafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu.

Walidai mabweni wanayotumia yamekuwa na matatizo mengi yanayosababisha chumba kimoja kutumiwa na wanafunzi wengi kutokana na uhaba uliopo.

Pia walidai madarasa yaliyopo hayakidhi mahitaji ya wanachuo waliopo. Baadhi yao wamelazimika kusomea kwenye bwalo la chakula. Ni kero kwao. Wanaiomba serikali kusaidia kuyakarabati na kuongeza madarasa mapya ili kuondokana na adha iliyopo.

Walidai chuo hicho kilichojengwa mwaka 1973, yaani miaka 50 iliyopita, kimekuwa kikidhalilisha wataalamu wengi sana wa afya hapa nchini lakini hakina uzio jambo ambalo linahatarisha usalama wa wanachuo na mali za chuo hicho.

"Tunaomba serikali kupitia Wizara ya Afya ikipe kipaumbele chuo kwenye masuala ya ukarabati na kuongeza kujenga madarasa kwani elimu bure imekuwa chachu kwa wazazi wengi kupeleka watoto shule na wengi wanapomaliza masomo yao ya sekondari wanakuwa hawana uwezo wa kuwapeleka vyuo vya binafsi ambavyo vina ada kubwa ambayo wazazi wetu wengi hawana uwezo wa kumudu gharama," alisema.

Mkuu wa chuo hicho, Dk. Godfrey Mdede alikiri kuwapo kero zinazolalamikiwa na wanachuo. Amewasilisha kero hizo wizarani na anaamini bajeti ya mwaka ujao wa fedha itakuwa na fungu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya chuo hicho.

Alisema kuwa baadhi ya kero zimekuwa zinatatuliwa kwa kutumia mapato yao ya ndani yanayotokana na ada za wanachuo kama kulipia maji, umeme, ukarabati mdogo na uendeshaji wa shughuli za kila siku.

Alibainisha kuwa chuo hicho kina uwezo wa kuchukua wanachuo zaidi ya 300 lakini kwa sasa kutokana na ubovu wa baadhi ya majengo na uchache wa vyumba vya madarasa, wanachukua wanafunzi 250.

HABARI KITAIFA

## Anayetuhumiwa kuua bila kukusudia apewa dhamana

Na Kulwa Mzee

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Mtwara, imekubali kumpa dhamana kwa masharti, Frank Chonjo, anayeshtakiwa kwa kuua bila kukusudia.

Uamuzi huo ulitolewa juzi mbele ya Jaji Eliamani Laltaika baada ya Mahakama kusikiliza maombi ya Chonjo.

Aliwasilisha maombi akiambatanisha na hati ya kiapo alichoapa Machi 28, mwaka huu akiomba mahakama imwachie kwa dhamana.

Katika hati ya mashtaka inadaiwa Oktoba mosi, 2022, maeneo ya Kijiji cha Chingulungulu wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara, mleta maombi alisababisha kifo cha Michael Samson.

Upande wa Jamhuri uliwasilisha kiapo kinzani kilichoapwa na Wakili wa Serikali, Florence Anyusisye, lakini wakati wa usikilizwaji wakili aliyekuwa akiiwakilisha Jamhuri, Melchior Hurubano aliomba kuiondoa hati ya kiapo kinzani na mahakama ilikubali.

Upande wa Jamhuri uliomba mahakama izingatie hoja walizowasilisha Aprili 5, mwaka huu.

Upande huo ulidai hakuna ubishi kwamba mwombaji anashtakiwa kwa kuua bila kukusudia na kosa hilo lina dhamana.

"Ni jukumu la mahakama kuhakikisha kwamba mwombaji akiwa nje kwa dhamana hataingilia upelelezi wa kesi," alidai.

Mahakama baada ya kusikiliza mawasilisho ilisema kwamba, mwombaji ataonekana ni mtu safi hadi pale atakapotiwa hatiani na mahakama ilikubali maombi yake.

Jaji Laltaika alitoa masharti kwa mwombaji awe na wadhamini wawili, kila madhamini atasaini dhamana ya maandishi ya Shilingi milioni tano, wawe na vitambulisho vinavyotambulika na mwombaji anatakiwa asifanye kosa lolote akiwa nje kwa dhamana.

**Uamuzi huo ulitolewa juzi mbele ya Jaji Eliamani Laltaika baada ya Mahakama kusikiliza maombi ya Chonjo.**

# Zanzibar yaripoti ongezeko mfumuko wa bei za bidhaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MFUMUKO wa bei wa mwezi Aprili 2023 umeongezeka na kufikia asilimia 1.85 kulinganishwa na asilimia 0.09 iliyoripotiwa mwezi Machi 2023.

Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za Bei katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Salma Saleh Ali, alibainisha hayo jana alipowasilisha takwimu za mwezi Aprili huko ofisini kwake Mazizini, Unguja.

Alisema mfumko wa bei wa bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kilevi kwa mwezi wa Apirili 2023 umeongezeka na kufikia asilimia 3.38 kulinganishwa na asilimia 0.67 iliyorekodiwa mwezi Machi 2023.

Alisema faharisi ya bei za jumla zimeongezeka na kufikia asilimia 106.24 kwa mwezi Aprili 2023 kulinganishwa na asilimia 98.84 iliyoripotiwa katika mwezi wa Aprili 2022.

Alitaja bidhaa zilizosababisha ongezeko la mfumuko huo ni pamoja na mchele wa mapembe (Rice Thailand) asilimia 3.6, mchele wa Mbeya asilimia 1.4, samaki asilimia 12.8, sukari asilimia 1.1, ndizi za mkono mmoja asilimia 33.2 na ndizi za mtwike asilimia 36.5.

Akizungumzia mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula, Salma alisema kuwa kwa mwezi Aprili 2023, ulifikia asilimia 11.52 kulinganishwa na asilimia 10.26 mwezi Machi 2023.

Ofisa huyo alisema faharisi za bei za bidhaa za chakula kwa mwezi Aprili 2023 zimeongezeka kufikia asilimia 111.81 kutoka asilimia 100.26 Aprili 2023, bidhaa zisizo za chakula zimeongezeka na kufikia asilimia 102.44 kwa mwezi Aprili 2023 kulinganishwa na asilimia 97.79 katika mwezi Aprili 2022.

Alisema mfumuko wa bei za bidhaa zisizo za chakula kwa mwaka umeshuka na kufikia asilimia 4.75 kwa mwezi Aprili 2023 kulinganishwa na asilimia 4.49 mwezi Machi 2023.

Mchumi kutoka Benki kuu ya Tanzania (BOT), Ulrick Mumburi, alisema Tanzania ipo vizuri katika mzunguko wa fedha na masuala ya bei kulinganishwa na nchi nyingine za Afrika.

Alisema kuwa kipindi cha mwezi wa Ramadhani, bei za bidhaa zilikuwa juu, jambo ambalo limesaidia uchumi na kupata mwelekeo mzuri wa bajeti ya mwaka.

Akitolea mfano wa nchi za Afrika, alisema mwezi Machi 2023, Kenya ulifikia asilimia 8.2 kutoka asilimia 7. 8 na Tanzania Bara ulifikia asilimia 4.8 kutoka asilimia 4.7.



Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Abeda Rashid (katikati), akizungumza wakati akifungua mafunzo ya walimu wa somo la usalama kwanza kwa askari polisi jana, watakaokuwa na jukumu la kutoa elimu ya udhalilishaji shuleni. Kulia ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, ACP Richard Mchomvu na Mratibu wa Programu ya Malezi Mbadala kutoka SOS, Nyenzuma Simai Issa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ACT-Wazalendo yaona upungufu bajeti kilimo

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema hakiridhishwi na usimamizi wa sekta ya kilimo na kumtaka Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kuweka wazi mikakati ya kuinua sekta hiyo kutokana na hotuba yake bungeni juzi kutoweka bayana mipango hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, Waziri Kivuli wa Sekta ya Kilimo, Mendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa chama hicho, Mtutura Abdallah, alisema ukuaji wa sekta hiyo bado ni mdogo katika kusukuma maendeleo ya eneo hilo.

"ACT-Wazalendo hakiridhishwi na usimamizi wa sekta ya kilimo katika kuelekea kufikia malengo ambayo imejiwekea yenyewe ikitaka ukuaji wa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

"Hotuba ya Waziri Bashe jana (juzi) huoni mtiririko wa mabadiliko katika lengo hilo. Kwa mfano mwaka 2021 kasi ya ukuaji wake ilikuwa asilimia 3.9. Waziri hajaiambia nchi mwaka huu wanatarajia kasi ya ukuaji wa kufikia asilimia ngapi. Hakulieleza Bunge tunafikaje asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

"Chama chetu kinakiweka kilimo katika vita ya kupambana na umaskini. Tanzania haiwezi kuondoa umaskini kwa kaulimbiu tu, bali kwa kuwa na muono wa wazi katika mipango ya kilimo. Sura ya umaskini wa watu ni kwa mkulima, tunahitaji kuongeza pato la mtu mmoja mmoja."

Kadhalika, chama hicho kilitaka serikali kununua chakula cha kutosha miezi mitatu.

"Katika hotuba ya Waziri Bashe alieleza nia ya serikali ya kuongeza uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) wa kununua chakula kutoka kwa wakulima kiasi cha tani 500,000 kama akiba.

"Hatua hii bado haitoshi kujiandaa na baa la njaa au kusaidia kukabiliana na mfumuko wa bei. Tunasisitiza serikali inunue na kuhifadhi chakula cha kutosha angalau cha miezi mitatu kutoka kwenye chakula kitakachovunwa mwaka huu ili kujilinda na upungufu wa chakula.

"Ukweli uko dhahiri kwamba maeneo mengi ya nchi uzalishaji wake unaweza kuwa sio mzuri kwa mwaka huu. Kwa hiyo kufanya hivyo kutasaidia NFRA kununua tani milioni 1.5 za mahindi, laki tano za mpunga na maharage tani milioni moja badala ya laki tano pekee."

Alisema changamoto iliyojitokeza katika usambazaji wa pembejeo na mbolea ya ruzuku mwaka 2022/2023 imechangia kwa kiasi kikubwa kupaa kwa bei ya vyakula kutokana na gharama za uzalishaji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JORDAN JOSEPH MWAKIPESILE** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya **TVS KING** yenye usajili namba: **MC525DCQ** na CHASSIS NAMBA: **MD6M14PA1M4H10596.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MBE/MBE/RB/110038/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 31/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMEDI ALLY wa Dodoma**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JAWA HUSSEIN HASSAN**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 08 Mwezi 05 Mwaka 2023.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI DODOMA

---

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ABDUKARIM RAJABU** KANJI MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA MAENEO YA TEMEKE – DAR ES SALAAM YENYE NO: **TAE 094916** ILIYOTOLEWA MAKAO MAKUU UHAMIAJI DAR ES SALAAM MWAKA: **2019** TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI CHA OYSTERBAY NA KUPEWA RB NO : **DAR/OST/RB/157583/2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 09/2023**

**In the Matter of the Estate of the ALLAN SAFARI KATONDO**

**And**

**In the Matter of the Application for Later of Administration by AINEA YOSIA KATONDO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grand of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before 31 day of May, 2023.

Dated at Korogwe this 02 day of April, 2023.

DISTRICT COURT
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MWALIMU RAMADHANI SUDI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 693 BJR – TOYOTA RAV 4.** Chassis namba **SXA1171585513.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/156220/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BASHARI RAMADHANI LEKULE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 435 BPH** Chassis No. **TRJ1205016484.** ENGINE No. **2TR157454 T435BPH TOYOTA LANDCRUISER PRADO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/158971/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASHA KIBIRA HANGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 499 CMD TOYOTA – RAV 4**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/33146/2023**

---

## KUPOTELEWA KWA LESENI YA UCHIMBAJI WA MADINI

**OMARI BARIADI MAPESA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA LESENI YA UCHIMBAJI MADINI YENYE NAMBA PML 0753 MBY.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/CHU/RB/149890/2023**

---

**FOMU MIRATHI – 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 680 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALLY MOHAMED KIDUME WA TANDIKA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MWEMA ALLY MOHAMED**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 05 Mwezi 06 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 08 Mwezi wa 05 Mwaka 2023.

HAKIMU

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **ALLY HUSSEIN MADIKAH** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya **(MITSUBISHI), CHASSIS NO. N23W5318013,** yenye namba za usajili **T 684 AAA.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **MOR/MOR/RB/157015/2023** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**Gaki Transport Co.LTD** Anatangaza kupotelewa na kadi mbili za gari aina ya Semi Trailer zenye namba za usajili **T.754 CFS na T.821 CFS.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na kampuni ya Gaki Transport kwa simu namba **0762-980232.** Taarifa ya Polisi.**SHI/SHI/RB/158716, 158717/2023.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA, LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA. 98 YA mwaka 2023**

**BENJAMIN F. OLEMOITA……………………………MDAI**

**VERSUS**

**MUSSA DAVID MALOGO…………………………MDAI WA 1**
**GRACE TENDEGA,………………………………,.….MDAIWA 2**

**KWA: GRACE TENDEGA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 12/05/2023 saa3:00 asubuhi.Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 14 ya mwezi wa APRIL mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA TANZANIA

---

FOMU MIRATHI – 2

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI**

**Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 690/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU BHUPENDRA J.BATAVIA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MAHASHWETA NARESH BATAVIA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wnaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 mwezi 05 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 05 mwaka 2023

---

**LAND DISPUTE COURTS (THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL)**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TUNDURU**

**MAHALI: TUNDURU**

**MAOMBI NO. 02/2021**

**FATUMA SELEMANI KIUTILA…………MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**CRDB BANK PLC**

**NEEMA KASILI NYALAGWINDA**

**MOSES ELIAS SHIREKA**

**MEM AUCTIONEERS AND GENERAL BROKERS LTD……MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: NEEMA KASILI NYALAGWINDA NA MOSES ELIAS SHIREKA**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa hukumu tarehe 26 mwezi Mei Mwaka 2023 saa mbili na nusu asubuhi mbele ya Mheshimiwa I.J. AYO Mwenyekiti wa Baraza.

Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 28 Mwezi April mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TUNDURU.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU ELIAS GRATION MUHIGI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina la **MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD** aina ya **BOXER BM 150** yenye namba za usajili **MC 505CFA.** Engine No. **PFZWKM83344,** Chasis No. **MD2A21BYXKWM88195.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/104624/2023.**

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Putin azitupia lawama nchi za magharibi

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Vladmiri Putin (pichani), amesema nchi za magharibi zina hila ya kuhakikisha nchi yake inaangamia.


Katika hotuba yake, kuadhimisha ushindi wa vita vya pili vya dunia dhidi ya Wanazi alisema lengo la nchi hizo sio kingine ila kuona kuporomoka kwa taifa lao.

Alisema kumbukumbu ya wale waliotetea nchi yao ni takatifu, huku akieleza kuwa vita vya kweli vinapigwa dhidi ya nchi yetu.

Putin, alisema Russia inataka siku zijazo zenye amani, huku akiwashutumu viongozi wa nchi za Magharibi kwa kupanda mbegu za chuki dhidi ya taifa lake.

Pia alisema anajivunia wanajeshi ambao wanashiriki katika kile anachokiita operesheni maalum ya kijeshi ya Russia nchini Ukraine.

Anasema hali ya Urusi na mustakabali wake inategemea watu hao na kwamba kila mtu ameungana kuunga mkono mashujaa wao.



Putin mara kwa mara anaifananisha serikali ya Ukraine iliyochaguliwa kidemokrasia na Wanazi walioshindwa katika Vita vya Pili vya Dunia.

Inaelezwa kuwa Putin anawashutumu viongozi wa Ukraine kama Wanazi mamboleo na kusema kuhusu vita vya kweli vinavyoendeshwa dhidi ya nchi ya Russia.

"Ni Russia pekee iliyosalia kweli kwa mafanikio ya Vita vya pili vya Dunia wakati nchi za Magharibi zimesahau ni nani aliyewashinda Wanazi," alisema.

Inabainishwa kuwa Warusi wamewahi kuambiwa kwamba walishinda Vita vya Pili vya Dunia, kwa hivyo haishangazi kwamba hajataja vita vya washirika ambavyo vilikomboa Ulaya ya Kusini na Magharibi dhidi ya Unazi. **BBC**

# Kesi ya kupinga uchaguzi Nigeria yaanza kusikilizwa

**ABUJA,** Nigeria

JOPO la majaji watano nchini Nigeria wamekaa kikao cha kwanza kusikiliza kesi inayowahusisha viongozi wa upinzani walioshiriki uchaguzi mkuu wa rais wa mwezi Februari ambao chama tawala kilishinda.

Tangu Nigeria irejee kwenye demokrasia mwaka 1999 miongo mitatu baada ya utawala wa kijeshi, uchaguzi umekuwa ukiishia mahakamani, ingawa hakuna pingamizi lililowahi kutengua matokeo.

Malalamiko ya kupinga ushindi wa Rais mteule Bola Tinubu yaliwasilishwa mwezi Machi pamoja na wagombea kadhaa wa urais akiwamo kiongozi mkuu wa upinzani Atiku Abubakar aliyeshika nafasi ya pili na mtu wa nje Peter Obi aliyeshika nafasi ya tatu.

**Katika ombi lake, Obi, ambaye aliungwa mkono kwa kiasi kikubwa na vijana wa Nigeria, pia alidai kushinda uchaguzi huo.**

Pia inaelezwa kuwa mahakama ina siku 180 za kutoa hukumu tangu maombi yalipowasilishwa, na pia ina uwezo wa kukata rufani katika mahakama ya juu zaidi.

Abubakar, ambaye alikuwa katika azma yake ya sita ya kuwania urais, alidai katika ombi lake kwamba alishinda uchaguzi huo uliofanyika Februari 25, mwaka huu.

Wote Abubakar na Obi walidai kuwa matokeo yaliyotangazwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kuwa ni batili kutokana na madai ya kutofuata sheria za uchaguzi na vitendo vya rushwa.

Abubakar, anayejulikana nchini Nigeria kama Atiku, pia alidai katika ombi lake la kurasa 223 kwamba Tinubu alishindwa kupata kizingiti cha kisheria cha asilimia 25 ya kura kutoka makao makuu ya nchi hiyo.

Katika ombi lake, Obi, ambaye aliungwa mkono kwa kiasi kikubwa na vijana wa Nigeria, pia alidai kushinda uchaguzi huo.

Hata hivyo mapambano yanayoendelea mahakamani hayawezi kuzuia kuapishwa kwa Tinubu Mei 29. Tinubu ni mrithi wa aliyekuwa Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari aliyekuwa madarakani kwa mihula miwili. **VOA**



Waziri Mkuu wa zamani wa Burundi, Alain Bunyoni, anayedaiwa kuzuiliwa jela kwa tuhuma za kuhatarisha usalama wa taifa hilo. **PICHA: MTANDAO**

# Mashambulizi ya anga yatikisa nchini Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

MASHAMBULIZI ya anga yameutikisa tena mji mkuu wa Sudan Khartoum katika kipindi mazungumzo ya Jeddah, Saudi Arabia yakionekana kama kutokuwa na matokeo yoyote muhimu.

Serikali ya Saudi Arabia ilisema pande zote mbili katika mzozo huo zinajiona kuwa zinaweza kushinda vita hivyo.

Sudan ilitumbukia katika machafuko mabaya baada ya kuzuka mapigano Aprili 15, mwaka huu, kati ya vikosi vya mkuu wa jeshi Abdel Fattah al-Burhan na naibu wake aliyegeuka mpinzani Mohamed Hamdan Daglo, anayeongoza Kikosi cha Msaada wa Dharura (RSF).

Inaelezwa kuwa mapigano yameua mamia, kujeruhi maelfu na kusababisha wengine wengi kuyakimbia makazi yao, hatua ambayo pia imezusha hofu yakuzorota kwa usalama hata nje ya mipaka ya Sudan.

Majenerali hao wanaopigana wametuma wawakilishi nchini Saudi Arabia kwa mazungumzo ya kuanzisha mapatano ya kibinadamu katika juhudi zinazoungwa mkono pia na Marekani. Na kwamba hadi juzi, majadiliano hayo yalionekana kutokuwa na matokeo yoyote.

Mwanadiplomasia mmoja aliyezungumza na Shirika la Habari la Ufaransa kwa masharti ya kutotajwa jina lake alisema "hakuna maendeleo makubwa, usitishaji vita wa kudumu hauko mezani. Kila upande unaamini kuwa unaweza kushinda vita."

Pia mapigano hayo yamesababisha wageni na hata Wasudan kulikimbia taifa hilo kwa kiwango kikubwa kwa kutumia usafiri wa nchi kavu, angani na hata baharini. Rawaa Hamad ambaye alifanikiwa kuondoka nchini Sudan kwa usafiri wa ndege hadi Qatar alisikika akisema "ni hatari sana kila mahali."

Inaelezwa kuwa alikuwa miongoni mwa abiria 71 aliyefika Qatar, ambako alisema raia nchini humo wanakabiliwa na matatizo ya ukosefu wa vingi muhimu vikiwamo maji, mafuta, dawa, hospitali na hata madaktari.

Mapigano katika mji mkuu na maeneo mengine ya nchi yameua zaidi ya watu 750 na kujeruhi zaidi ya 5,000.

Aidha, taarifa mpya ya Jumuiya ya Madaktari wa Sudan iliyojikita katika jimbo la Darfur ilibainisha kuwa mapigano hayo yamesababisha vifo vya watu takriban 100, huku ikieleza kuwa kumekuwa na shida ya huduma katika vituo vya tiba katika mji mkuu wa jimbo hilo Genena.

Pia kutokana na vurugu hizo inaelezwa kuwa kumekuwa na shida ya kupata takwimu za walioajeruhiwa hadi sasa.

Idadi ya vifo vya chama hicho inatolewa katika kipindi hiki ambacho kumekuwapo na mazungumzo yakiendelea kati ya pande zinazopingana katika mji wa Jeddah nchini Saudi Arabia.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Saudi Arabia ilisema mazungumzo hayo yaliyoanza juzi yanayohusisha jeshi kwa upande mmoja na mwingine kwa wanamgambo wenye nguvu yanatarajiwa kuendelea kwa siku kadhaa.

Inaelezwa kuwa tangu kupanga mapinduzi ya Oktoba 2021 ambayo yalisimamisha serikali ya mpito ya utawala wa kiraia, Burhan na Daglo walianguka katika vita vya kuwania madaraka. **DW**

HABARI MICHEZO

# WABUNGE, MACHIFU DIMBANI KUCHANGIA MATIBABU SARATANI

Na Restuta James

WABUNGE na machifu wanategemea kuwa na mechi ya mpira wa miguu ya 'kukata na shoka' itakayopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Mei 27, mwaka huu, ikiwa na lengo la kukusanya Sh. milioni 300 kwa ajili ya kuchangisha matibabu ya wagonjwa 100, wanaougua ugonjwa wa saratani.

Kabla ya mchezo huo wananchi watapata fursa ya kufanya uchunguzi wa awali wa magonjwa yasiyoambukiza, ukiwamo wa saratani kuanzia Mei 25 hadi Mei 28, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Machifu Tanzania, Antonia Tomisiza, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa nia ya mechi hiyo ni kusaidia juhudi za serikali katika kuwahudumia wagonjwa wa saratani.

**Alisema: "Tunaomba wananchi, mashirika, kampuni na sekta binafsi kushiriki katika kuchangia matibabu kwa kuwa wagonjwa wengi hawana uwezo."**

Kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema ugonjwa huo bado ni tatizo nchini huku takwimu za hivi karibuni zikieleza kuwa Tanzania inapata wagonjwa wapya 42,046 kila mwaka.

Alisema saratani ya shingo ya kizazi inaongoza miongoni mwa saratani 10 zinazowashambulia watu nchini ikifuatiwa na saratani ya matiti.

Dk. Mwaiselage alitaja saratani nyingine nane zinazowashambulia watu nchini ni ya njia ya chakula kooni, saratani ya kichwani na shingo, kaposi sarcoma, tezi dume, thyroid, utumbo mpana, lymphoma na saratani ya damu.

"Saratani ya matiti imeongezeka sana, ilikuwa namba nne, lakini sasa ndiyo inaongoza. Saratani ya tezi dume nayo haikuwamo kwenye hizi 10, lakini sasa ni ya sita," alisema.

Alisema serikali ndiyo inabeba gharama za matibabu ya saratani kwa asilimia kubwa na kwamba uchunguzi hadi tiba ya mgonjwa mmoja ni Sh. milioni tatu.

Dk. Mwaiselage, aliitaka jamii kuchangia matibabu ya wagonjwa katika programu ya Chifu na Huduma Jamii, kupitia akaunti ya Taasisi ya Saratani Ocean Road namba 20101100166 iliyopo Benki ya NMB.

MAZOEZI...



Mwanariadha wa Tanzania, Omari Maulidi 'Pengo' (kushoto) na Florian Zittel kutoka nchini Ujerumani, wakifanya mazoezi ya kukimbia katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Diarra kinara wa 'clean sheets' 2022/23

Na Adam Fungamwango

KIUNGO mshambuliaji wa Klabu ya Yanga, Stephane Aziz Ki, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi Aprili wa Ligi Kuu huku kipa wa timu hiyo, raia wa Mali, Djigui Diarra, akiwa ndiye kinara wa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao 'clean sheets' kwa msimu wa 2022/23.

Licha ya msimu huu wa 2023, kubakisha mechi tatu kwa kila timu kabla ya kumalizika, Kipa huyo wa Yanga, Diarra, ndiye kinara wa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao kutokana na kuwa na 'clean sheets' 16 ambazo haziwezi kufikiwa na kipa yeyote yule.

Kwa mujibu wa rekodi za Ligi Kuu, kipa wa Simba, Aishi Manula anayefuata kwa karibu ana clean sheets 12, na ameripotiwa kuwa hatocheza mechi zilizosalia za msimu huu na hata kama angecheza na kutoruhusu bao angeishia na 15.

Katika hatua nyingine, taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi imesema Azizi Ki ndiye mchezaji bora wa Ligi Kuu kwa mwezi Aprili na kwamba uchaguzi huo umetokana na kikao cha Kamati ya Tuzo za Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kilichokutana jijini Dar es Salaam Jumamosi ya Mei 6, mwaka huu, pia kikimchagua Kocha Mkuu wa Prisons, Abdallah Mohamed 'Bares', kuwa kocha bora wa mwezi huo.

Kiungo huyo mshambuliaji raia wa Burkina Faso aliwashinda straika Mkongomani wa Simba, Jean Baleke na Ayoub Lyanga wa Azam FC ambao aliingia nao fainali.

Katika mechi zake mbili alizocheza, Aziz Ki alitumia dakika 135, akifunga mabao matatu na pasi ya mwisho moja.

Kwa upande wa Bares, aliwashinda Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira na Daniel Cadena wa Azam ambao waliishia hatua ya fainali.

# Simba, Yanga Veterani wataka mechi kila mkoa

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kumalizika kwa mechi yao iliyofana kati ya wachezaji wa zamani wa timu za Simba na Yanga kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha Jumamosi iliyopita, baadhi yao wametaka ikiwezekana kipute kama hicho kipelekwe kila mkoa Tanzania Bara na Visiwani kwa ajili ya kuwapa nafasi mashabiki ambao hawakuwahi kuwaona, sasa kuwashuhudia mubashara badala yake kuwasikia tu redioni.

Straika wa zamani wa Klabu ya Simba, Joseph Kaniki 'Golota', aliisifu Kampuni ya Maji ya Kilimanjaro, ITV/Redio One na Smart Gin kwa kudhamini na kufanikisha mechi hiyo iliyovutia si mashabiki tu waliojazana Uwanja wa Sheik Amri Abeid jijini Arusha, hata wao wachezaji, hivyo kuomba kama inawezekana baada ya Arusha, wakacheze kwenye mkoa mwingine, na iendelee ikiwezekana hadi kumalizika kwa mikoa yote.

"Binafsi, nilijisikia raha sana kwa sababu nimekutana na watu ambao mara ya mwisho nilionana nao miaka 10 iliyopita, kwa hiyo tunaomba mechi kama hizi kama vipi ziwe zinachezwa mara kwa mara kwenye mikoa tofauti ili kuwapelekea mashabiki uhondo na baadhi ya watu wakawaone wachezaji wa zamani ambao kipindi hicho walikuwa wadogo na kuwasikia tu kwenye redio.

"Na hata sisi wenyewe tuweze kukutana na kubadilishana mawazo, ikizingatiwa baadhi yao kwa sasa ni makocha tunaweza kusaidiana hili na lile," alisema straika huyo aliyesifika kuwa na nguvu na mashuti makali.

Winga machachari wa zamani wa Yanga, Edibilly Lunyamila, alisema kwenye mechi za Simba na Yanga huwa hakuna dogo kwani hata waliocheza, ilipata baraka kutoka viongozi wa klabu hizo.

"Simba na Yanga huwa hazipotei na hazipotezi ushindani, watu walishuhudia uwanjani, wanakamiana kama kawaida, mambo mengi, lakini tukishamaliza tunakuwa marafiki," alisema.

George Masatu, beki wa kati wa zamani wa Simba, mbali na kuomba kipigwe tena, alishangaa kuona mechi hiyo ikiwa na upinzani mkali kuliko alivyotegemea.

"Nimekumbuka miaka yetu tulipokuwa tunakutana na hawa mabwana, mimi mwanzo nilidhani mechi itakuwa ya kawaida tu, kumbe haikuwa ya kitoto ni mechi kweli kama vile tulivyokuwa tumecheza Simba na Yanga za enzi zile, ilikuwa kama ndiyo tunacheza Ligi Kuu ya msimu huu halafu tumekutana wenyewe," alisema Masatu aliyekuwa akisifika kwa kuokoa mipira iliyokuwa inakwenda kutinga wavuni.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### MESSI, AL HILAL BADO

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi, 35, ambaye mkataba wake na PSG unamalizika majira ya joto, bado hajafikia makubaliano ya kujiunga na klabu ya Al Hilal ya Saudi Arabia na mchezaji huyo hatarajiwi kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake hadi mwisho mwa msimu. ***(Mundo Deportivo)***

#### MOURINHO ATAKIWA PSG

MSHAURI wa Paris St-Germain, Luis Campos, amezungumza na wakala wa Jose Mourinho kuhusu uwezekano wa kocha huyo wa AS Roma kujiunga na klabu hiyo ya Ufaransa msimu huu wa majira ya joto. ***(RMC Sport)***

#### OSIMHEN AWANIWA CHELSEA

CHELSEA inatazamia kumtoa mshambuliaji wa Marekani, Christian Pulisic, 24, mwishoni mwa msimu huu na wanaweza kumtumia kama chambo cha kuwashawishi mabingwa wa Italia Napoli kuwauzia mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, 24. ***(Mail)***

#### RAPHINHA EURO MIL. 80

KLABU ya Barcelona imeweka bei inayotakiwa ya euro milioni 80 kwa winga wa Brazil, Raphinha, 26, huku Newcastle United na Chelsea zikitaka kumrejesha mchezaji huyo wa zamani wa Leeds United kwenye Ligi ya England. ***(Sport)***

#### XHAKA ANYATIWA LIVERKUSEN

KLABU ya Ujerumani Bayer Leverkusen imefufua nia yake ya kumnunua kiungo wa kati wa Arsenal, Granit Xhaka, 30, baada ya kujaribu kumsajili kiungo huyo wa Uswisi msimu uliopita. ***(Mirror)***

#### RICE BADO HAKIELEWEKI

WEST Ham haijavutiwa na mchezaji anayetumika kama sehemu ya ofa yoyote kwa kumpata kiungo wa kati wa England, Declan Rice, 24, bali wanataka thamani yao ya pauni milioni 100 kufikiwa ikiwa watamruhusu mchezaji huyo kuondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

#### GUENDOUZI NA WEST HAM

KIUNGO wa kati wa Marseille na Ufaransa, Matteo Guendouzi, 24, ananyatiwa na West Ham kwani wanamwona mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal kama mbadala wa nahodha wao, Declan Rice. ***(Athletic)***

#### MUANI BEI JUU SOKONI

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Randal Kolo Muani, atagharimu angalau euro milioni 90 kwa klabu yoyote inayotaka kumsajili mchezaji huyo kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa Eintracht Frankfurt, Axel Hellmann, 24. ***(90 Min)***

#### PALACE YAMTAKA OLISE

WINGA wa Crystal Palace, Michael Olise, 21, anawavutia wababe wa Ligue 1, Paris St-Germain, ambao wako tayari kuwasilisha ofa ya kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa chini ya umri wa miaka 21 msimu huu wa majira ya joto. ***(Mail)***

#### DEMBELE AWINDWA EPL

KLABU za Aston Villa, Leeds United na West Ham zimehusishwa na mshambuliaji wa Lyon, Mfaransa Moussa Dembele, 26, ambaye aliwahi kuzichezea Fulham na Celtic. ***(Birmingham Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AWASHIWA TAA ZA KIJANI KUONDOKA PSG

**PARIS,** Ufaransa

● ● ● Takriban mashabiki 50 wa klabu hiyo wamekwenda nyumbani kwake wakitaka...

NEYMAR yuko tayari kuondoka Paris Saint-Germain msimu huu wa majira ya joto licha ya kuwa bado ana miaka minne kwenye mkataba wake, vyanzo vimeiambia ESPN, na klabu hiyo imeridhia kumwachia ikiwa ofa sahihi itapatikana.

**Mabingwa hao wa Ligue 1 walijaribu kumtafutia klabu msimu uliopita wa majira ya joto, lakini hawakuweza kupata ofa yoyote ya maana kwa namba 10 huyo.**

Nyota huyo, ambaye alitimiza umri wa miaka 31 Februari na anapata nafuu kutokana na upasuaji wa kifundo cha mguu, hakutaka kuondoka katika mji mkuu wa Ufaransa wakati huo, lakini vyanzo vimesema amebadilisha mawazo yake katika wiki za hivi karibuni na amefungua mlango wa uwezekano wa kuondoka.

Takriban mashabiki 50 wa PSG walikwenda nyumbani kwa Neymar wiki iliyopita wakitaka aondoke katika klabu hiyo.

Vyanzo vya habari vilisema Neymar alikuwa na mabadiliko moyoni kama anataka kusalia Paris au la, huku vikiongeza kuwa hajisikii kukaribishwa tena na anafikiria kuwa itakuwa bora kucheza mahali pengine msimu ujao.

Aidha, vyanzo hivyo vya habari vilisema kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil angependelea kuhamia Ligi Kuu England, nyumbani kwa timu chache ambazo zinaweza kumudu kulipa mshahara wa Neymar wa Euro milioni 40 kwa mwaka na kugharamia kile ambacho kinaweza kuwa ada kubwa ya uhamisho.

PSG ililipa Barcelona kiasi cha euro milioni 222 katika msimu wa majira ya joto wa 2017 ili kumpata Neymar.

Mwenyekiti wa PSG, Nasser al Khelaifi alikutana na mmiliki mpya wa Chelsea, Todd Boehly, Februari mwaka huu kujadili uwezekano wa kumnunua Neymar.

Wawili hao wamezungumza kuhusu Neymar, kulingana na vyanzo, ambavyo viliongeza kuwa Boehly ni shabiki mkubwa wa Neymar na angependa kumuona Stamford Bridge.

Neymar hatafikiria kurejea kwao Brazil kwa wakati huu na hayuko tayari kuchezea klabu yoyote nchini Hispania isipokuwa Barcelona, ambayo haina mpango wa kumsajili nyota wao huyo wa zamani.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,112,46

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 10,11 NA 12 MEI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 10/05/23 | 22:00 | AC Milan vs Inter | 2.96 | 3.01 | 2.39 |
| 02. 11/05/23 | 01:00 | Coquimbo vs Univ de Chile | 2.58 | 3.32 | 2.43 |
| 03. 11/05/23 | 02:00 | Rangers vs San Luis Quillota | 2.64 | 3.00 | 2.58 |
| 04. 11/05/23 | 02:00 | FC Cincinnati vs New York City | 2.24 | 3.47 | 2.74 |
| 05. 11/05/23 | 03:30 | Cruzeiro vs Fluminense | 2.83 | 3.22 | 2.29 |
| 06. 11/05/23 | 05:30 | LA Galaxy vs Seattle Sounders | 2.44 | 3.21 | 2.64 |
| 07. 11/05/23 | 16:00 | Pontedera vs AC Siena | 2.37 | 2.78 | 3.04 |
| 08. 11/05/23 | 19:00 | Sonderjyske vs Vejle BK | 2.72 | 3.39 | 2.23 |
| 09. 12/05/23 | 01:00 | Coritiba vs Vasco da Gama | 2.40 | 3.17 | 2.72 |
| 10. 12/05/23 | 01:00 | Botafogo RJ vs Corinthians | 2.14 | 3.21 | 3.12 |
| 11. 12/05/23 | 01:00 | Univ de Concepcion vs Antofagasta | 2.85 | 2.96 | 2.43 |
| 12. 12/05/23 | 13:30 | FC Tokyo vs Kawasaki Frontale | 2.83 | 3.19 | 2.26 |
| 13. 12/05/23 | 19:00 | Slaven Belupo vs Lokomotiva Zagreb | 2.51 | 3.09 | 2.57 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GREENWOOD KUTUA JUVE KWA MKOPO




**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus inaripotiwa kuwa tayari kutoa ofa ya kumsajili kwa mkopo Mason Greenwood kutoka Manchester United.

Mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, bado haujulikani na tetesi zinaendelea kuzagaa kuhusu ofa kutoka nje ya nchi.

Anaendelea kufungiwa na klabu huku wakifanya uchunguzi wa ndani kuhusu tuhuma za ubakaji zinazomkabili.

Greenwood alikamatwa Januari 2022 baada ya tuhuma za kujaribu kubaka na kushambulia, lakini mashtaka dhidi yake yalitupiliwa mbali Februari 2023.

Bado hajarejea kufanya mazoezi na klabu hiyo na inadhaniwa kuwa anaweza kufanya hivyo mwanzoni mwa msimu ujao.

Gazeti la The Sun limeripoti kuwa Juventus wamepiga hatua kwenye kambi ya Greenwood juu ya uwezekano wa kumsajili kwa mkopo wa muda mrefu.

Mchezaji mwenzake wa zamani, Paul Pogba, yumo kwenye kikosi hicho na inatumainiwa kuwa anaweza kubadili mambo kwa upande wa Serie A. Pia AC Milan na Roma wanadaiwa kuvutiwa naye.



# *Kompany azawadiwa miaka mitano Burnley*

**LONDON,** England

KLABU ya Burnley imemzawadia Kocha wao, Vincent Kompany, mkataba mpya wa miaka mitano baada ya kuipandisha timu hiyo kutoka Ligi ya Championship hadi Ligi Kuu England, EPL.

Beki huyo wa zamani wa Manchester City aliipandisha timu hiyo hadi EPL katika msimu wake wa kwanza wa kuwa kocha kwenye dimba la pale Turf Moor.

Amekuwa akihusishwa na nafasi nyingi za ligi kuu zikiwamo Chelsea na Tottenham Hotspur, lakini sasa ameweka mustakabali wake kwa Clarets hao hadi mwaka 2028.

Mbelgiji huyo alisema: "Burnley walijisikia vizuri tangu mwanzo kwa hiyo ninahisi sawa kusaini miaka mitano ijayo.

"Pamoja na mashabiki tumeufanya Uwanja wa Turf Moor kuwa ngome tena na tunaendelea kutazamia siku zijazo na kazi ya kuifanya Burnley kuwa bora kwa kila hatua."

Kompany alichukua n fasi ya Sean Dyche maji ya joto yaliyopita baad ya klabu hiyo kushuka d raja.

Mwenyekiti Alan Pac aliongeza: "Tuna furah kwamba Vincent am saini mkataba mpya. Yey ndiye anayefaa kabi kwa jinsi sote tunaon Burnley ikisonga mbele.

"Kiongozi wa ajab anayeweka viwango vy juu zaidi na kuipelel klabu yetu katika viwang ambavyo sote tunatal kufikia."

HABARI MICHEZO

62,859/-

# AZAM: TUNAUTAKA UBINGWA FA

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Klabu ya Azam FC, umeweka wazi kuwa unauhitaji ubingwa wa Kombe la Shirikisho la Soka nchini, maarufu FA Cup, na wataelekeza nguvu kwenye mchezo wao wa fainali.

Azam wametinga fainali ya michuano hiyo baada ya kuitupa nje Simba kutokana na ushindi wa mabao 2-1 walioupata katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara mwishoni mwa wiki iliyopita.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Afisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema sababu kubwa ya kuutaka ubingwa huo ni kutokana na ukweli kuwa hawana nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu.**

Alisema ushindi walioupata dhidi ya Simba umewapa mzuka zaidi wa kujipanga kuhakikisha hawatoki kapa msimu huu kama ilivyokuwa msimu uliopita.

"Kombe la Shirikisho la Azam ndio pekee ambalo tunaweza kugombania, tunasubiri nusu fainali ya pili kati ya Yanga na Singida Big Stars ili tujue tutakutana na nani, kama Azam FC tuna malengo ya kutwaa ubingwa huu," aliseama Popat.

Alisema wachezaji wake walifanya kazi kubwa kwenye mchezo dhidi ya Simba na kuwafanya kusonga mbele.

"Sio kazi ndogo kuitoa kwenye mashindano timu kama Simba, walikuwa kwenye mashindano ya kimataifa na wana kikosi kizuri, Azam tumeonesha ukomavu na ubora wa kikosi chetu, tunawapongeza wachezaji wetu," alisema Popat.

Aidha, alisema wapo tayari kukutana na timu yoyote kati ya Yanga ama Singida Big Stars.



Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Tanga, Ramadhani Omari (watatu kushoto), akimkabidhi mpira kwa mchezaji wa Timu ya Damuni FC, wakati akifungua Tawi la Wakereketwa la Vijana wa UVCCM juzi, katika mtaa wa Masuguru, Muheza ambapo pia alifungua tawi jingine mtaa wa Shauri Moyo Mdote Kata ya Majengo huku akiwataka vijana kupambana katika kupiga vita ushoga na ndoa za jinsia moja. Wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa UVCCM wilayani Muheza Aziza Mshakangoto na Watatu ni Katibu wa UVCCM Mkoa wa Tanga, Theresia Makyao. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Robertinho aanika majembe

INATOKA UK. 23

wa usajili utaanza mapema na utakuwa wa kishindo kutokana na jinsi msimu huu ullivyokuwa mbaya kwetu, tumemaliza msimu salama licha ya kuwapo kwa mechi tatu na tutashiriki vema na kumaliza msimu vizuri kwa heshima.

"Kila shabiki anaumizwa na matokeo ya Simba msimu huu, tunaheshimu maumivu ya kila Mwanasimba, kikubwa ni kuangalia msimu huu na kujipanga kwa msimu ujao, kukosa ubingwa mfululizo si la kuogopesha, kuna timu nyingine nje ambazo zilikuwa na mafanikio, kwetu ni somo kwa Wanasimba kujipanga kwa ajili ya msimu ujao na kuboresha kikosi," alisema Ahmed.

Aliongeza anaungana na mashabiki wanaotaka viongozi kufanya usajili bora, kwani mafanikio ya mpira unajikita katika usajili na hilo limewafanya msimu huu kushindwa kufikia malengo yao.

"Tulipofeli na kuanguka ni pale tuliposajili watu ambao tulitegemea watafanya vizuri, hatimaye haikuwa hivyo na tunaelekea katika usajili na viongozi wanatakiwa kuwa makini kwenye usajili kwa kuboresha kikosi kwa msimu ujao," alisema Ahmed.

## Nabi aonya

INATOKA UKURASA 24

asipigiwe kelele kwa sababu hii mechi si rahisi kama wanavyofikiri, tutapambana na kupata matokeo mazuri," alisema Nabi.

Mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Metacha Mnata, alisema maandalizi yamekamilika na wanajiandaa kuhakikisha wanaweka historia kwa Tanzania kuvuka hatua ya nusu na kuwa sehemu ya historia ya kucheza fainali.

"Hii ni mechi ngumu na tunatakiwa kupata matokeo mazuri na tunahitaji kupata matokeo mazuri uwanja wa nyumbani ili mechi ijayo ya marudiano tusicheze kwa presha kubwa," alisema Metacha.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/05/23 | 17:00 | Aston Villa vs Tottenham Hotspur | 2.18 | 3.40 | 2.95 |
| 02. 13/05/23 | 17:00 | Southampton FC vs Fulham FC | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 03. 13/05/23 | 17:30 | FC Vizela vs FC Famalicao | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 04. 13/05/23 | 19:15 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 2.65 | 3.15 | 2.24 |
| 05. 13/05/23 | 19:30 | Sunderland AFC vs Luton Town | 2.60 | 3.20 | 2.60 |
| 06. 13/05/23 | 19:30 | Villarreal CF vs Athletic Bilbao | 2.17 | 3.35 | 3.00 |
| 07. 13/05/23 | 19:45 | FC Volendam vs Sparta Rotterdam | 2.85 | 3.45 | 2.24 |
| 08. 13/05/23 | 21:30 | CA Independiente Avellaneda vs CA Tigre | 2.44 | 2.90 | 2.60 |
| 09. 14/05/23 | 00:00 | CA Banfield vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.47 | 2.80 | 2.65 |
| 10. 14/05/23 | 13:30 | Hellas Verona vs Torino FC | 2.29 | 3.05 | 3.10 |
| 11. 14/05/23 | 14:00 | Coventry City vs Middlesbrough FC | 2.70 | 3.25 | 2.42 |
| 12. 14/05/23 | 15:00 | RC Celta de Vigo vs Valencia CF | 2.16 | 3.20 | 3.20 |
| 13. 14/05/23 | 16:30 | VfB Stuttgart vs Bayer Leverkusen | 2.60 | 3.40 | 2.43 |
| 14. 14/05/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 15. 14/05/23 | 18:05 | AS Monaco vs Lille OSC | 2.60 | 3.50 | 2.37 |
| 16. 14/05/23 | 19:00 | Bologna FC vs AS Roma | 3.15 | 3.00 | 2.28 |
| 17. 14/05/23 | 20:00 | Defensa y Justicia vs Estudiantes de La Plata | 2.26 | 2.85 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 10/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1414 | Suwon Samsung vs Jeonbuk Hyundai | 2.98 | 3.13 | 2.20 |
| 13:30 | 1654 | Jeju Utd vs Incheon Utd | 2.20 | 3.13 | 2.98 |
| 13:30 | 1778 | Urawa Red Diamonds vs Sagan Tosu | 1.53 | 3.90 | 5.03 |
| 13:30 | 1793 | Daejeon Citizen vs Suwon City | 2.00 | 3.38 | 3.18 |
| 14:35 | 1767 | Nantong Zhiyun vs Hangzhou NG | 2.71 | 3.07 | 2.41 |
| 14:35 | 2470 | Changchun Yatai vs Meizhou Kejia | 1.90 | 3.33 | 3.54 |
| 14:35 | 2725 | Shanghai SIPG vs Qingdao Hainiu | 1.29 | 4.73 | 8.23 |
| 14:35 | 3443 | Beijing Guoan vs Tianjin Teda | 1.93 | 3.18 | 3.60 |
| 14:35 | 5745 | Chengdu Qianbao vs Shandong Luneng | 2.55 | 3.14 | 2.50 |
| 15:00 | 4869 | Maktaaral vs Astana | 7.43 | 4.34 | 1.34 |
| 15:30 | 1283 | FC Samtredia vs Dinamo Batumi | 7.21 | 4.53 | 1.35 |
| 15:30 | 3092 | Merani Martvili vs Loko Tbilisi | 1.71 | 3.63 | 4.15 |
| 15:50 | 2025 | AL Ain vs AL Hazm | 4.05 | 3.18 | 1.82 |
| 16:00 | 1082 | AS Oued Ellil vs Avenir S Marsa | 3.18 | 2.57 | 2.46 |
| 16:00 | 1199 | Stade Gabesien vs SS Sfaxien | 1.65 | 3.29 | 5.04 |
| 16:00 | 1241 | SC Moknine vs EGS Gafsa | 3.45 | 2.75 | 2.07 |
| 16:00 | 1546 | Avenir Sportif Gabesien vs CO Mednine | 1.90 | 2.75 | 4.00 |
| 16:00 | 2023 | AS Djerba vs Club S Hammam-Lif | 5.20 | 2.80 | 1.68 |
| 16:00 | 2213 | Township Rollers vs Eleven Angels | 1.49 | 3.93 | 5.78 |
| 16:00 | 2443 | EM Mahdia vs Js Omrane | 2.16 | 2.75 | 3.15 |
| 16:00 | 3012 | ES Jerba Midoun vs CS Korba | 1.73 | 3.02 | 5.01 |
| 16:00 | 3100 | Young Africans vs Marumo Gallants FC | 1.69 | 3.24 | 4.81 |
| 16:00 | 4428 | Police XI vs Orapa United | 4.46 | 3.42 | 1.71 |
| 16:00 | 5456 | Galaxy FC vs Nico United | 1.40 | 4.23 | 6.61 |
| 17:15 | 1034 | Shahrdari Astara vs Fajr Sepasi | 3.67 | 2.69 | 2.19 |
| 17:15 | 1184 | Saipa Karadj vs Khosheh Talaei | 2.03 | 2.75 | 4.10 |
| 17:15 | 1880 | Vanpars vs Arman Gohar Sirjan | 1.75 | 2.80 | 4.80 |
| 17:15 | 3180 | Chador Malu Yazd vs Chooka Talesh FC | 1.72 | 3.12 | 5.09 |
| 18:00 | 1557 | FC Telavi vs Shukura | 2.09 | 3.12 | 3.33 |
| 18:00 | 1655 | FK Tikves Kavadarci vs FK Skopje | 1.96 | 2.95 | 3.98 |
| 18:00 | 2111 | Shkupi Skopje vs Makedonija GjP | 1.26 | 4.50 | 8.20 |
| 18:00 | 2701 | Shkendija vs FC Struga Trim Lum | 2.01 | 2.90 | 3.88 |
| 18:00 | 3269 | Ararat Armenia vs Alashkert Martuni | 1.92 | 3.35 | 3.56 |
| 18:00 | 3329 | Bregalnica Stip vs Akademija Pandev | 2.35 | 2.85 | 2.75 |
| 18:00 | 3967 | Sileks vs Rabotnicki Sk | 2.25 | 2.80 | 2.95 |
| 18:15 | 2010 | AL Sahel SC vs Najran SC | 2.16 | 2.85 | 3.05 |
| 19:00 | 1982 | AL Baten vs AL Tai | 3.19 | 3.57 | 2.10 |
| 19:00 | 3332 | Ida-Virumaa FC Alliance vs FC Elva | 5.52 | 4.99 | 1.45 |
| 19:00 | 3962 | Karlovy Vary vs Loko Vltavin | 2.57 | 3.29 | 2.40 |
| 19:00 | 5519 | Aali vs AL Ittihad Bhr | 1.76 | 3.52 | 4.04 |
| 19:00 | 5867 | Pisek vs Kraluv Dvur | 1.85 | 3.49 | 3.54 |
| 19:15 | 4045 | Al Faisaly (KSA) vs Al Qadisiyah | 1.77 | 3.09 | 4.53 |
| 19:20 | 1762 | AL Khlood vs AL Akhdood | 3.25 | 2.89 | 2.20 |
| 20:00 | 4477 | ASEC Mimosas vs USM Alger | 1.99 | 3.00 | 3.64 |
| 20:30 | 3001 | Orleans vs Le Mans | 2.15 | 3.15 | 3.31 |
| 21:00 | 5805 | Chelsea W vs Leicester City FC W | 1.07 | 8.93 | 18.70 |
| 21:30 | 1452 | Brighton and Hove Albion W vs Arsenal W | 11.40 | 6.01 | 1.18 |
| 22:00 | 5613 | AC Milan vs Inter | 2.90 | 3.05 | 2.39 |
| 22:30 | 1768 | Santiago Wanderers vs San Marcos | 2.01 | 3.01 | 3.69 |
| 23:00 | 4822 | America vs Guayaquil SC | 2.07 | 3.17 | 3.32 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Mei 10, 2023

Nipashe




## Neymar awashiwa taa kuondoka PSG

UKURASA 21

TUPO TAYARI...




Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi, (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana kuhusu mchezo wao wa mkondo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini utakaopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo, kulia ni kipa wa timu hiyo, Metacha Mnata. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nabi aonya, Marumo ikiapa kula na Mayele

## ●●● Ataja mbinu za kushambulia huku Kocha Kerr akisema wamefuata...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, akiionya timu yake kwa kutoa tahadhari ya namna ya kuimaliza mechi ya mkondo wa kwanza ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Galants leo, wapinzani wao hao wamewataja nyota wa kuchungwa wakianza na mshambuliaji Fiston Mayele.

**Yanga itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo saa 10:00 alasiri kuikaribisha Marumo Gallants, ikidhamiria kupata ushindi mnono nyumbani kabla ya timu hizo kurudiana wiki ijayo nchini Afrika Kusini.**

Hata hivyo, wakati nguzo kuu ya Yanga katika safu ya ushambuliaji ikiwa ni Mayele, Kocha Mkuu wa Marumo Gallants FC, Dylan Kerr, amekiri ubora wao katika safu ya ushambuliaji na kueleza watahakikisha wanawachunga nyota wote hatari wa wapinzani wao akiwamo mshambuliaji huyo, Stephane Aziz Ki na wengine.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Marumo Gallants FC, Raymond Mdaka, alisema wamefanya maandalizi kulingana na mechi iliyopo mbele yao leo na kwamba wamejiandaa na wako tayari kwa kuwakabili Yanga.

“Hatuwezi kuwaongelea sana wapinzani wetu kwa sababu unaweza kusahau, ila tumefanya maandalizi mazuri dhidi ya Yanga kupata matokeo mazuri ugenini,” alisema kocha huyo.

Nahodha wa Marumo Gallants FC, Washington Arubi, alisema wamejiandaa na wanafahamu Yanga ni timu kubwa na watacheza kwa tahadhari kubwa.

“Hatutaangalia mchezaji mmoja Mayele (Fiston), bali tumekuja kucheza na Yanga, tumekuja kucheza mpira na si kuangalia au kuwachunga baadhi ya wachezaji bali tunahitaji kufanya vizuri, ugenini,” alisema Arubi.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nabi alisema maandalizi yameenda, kama walivyopanga na wamewasoma wapinzani wao baada ya kuona baadhi ya michezo waliyocheza ya ligi yao na mechi za kimataifa.

Alisema wachezaji wako na ari kubwa ya kwenda kupambana na kuwa tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi mkubwa dhidi ya wapinzani wao hao.

“Niwapongeze Marumo Gallants, ni timu nzuri licha ya kwamba katika ligi yao hawafanyi vizuri, lakini kwenye mashindano haya wamefanya vizuri na wamezitoa timu kubwa hapa Afrika ikiwamo Pyramids ya Misri.

“Hadi kufika hapa Marumo Gallants, si kwa bahati mbaya, moja ya timu ambayo tunatakiwa kucheza nayo kwa umakini mkubwa kutokana na matokeo yao ya mechi za kimataifa, kila mechi wamefanikiwa kufunga,” alisema Nabi.

Aliongeza kuwa mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu wanacheza dhidi ya timu bora, na hawataibeza kwamba wanaweza kuifunga kwa urahisi.

“Hii timu unatakiwa kucheza nayo kwa akili ya hali ya juu na si mechi ya kushambulia shambulia tu kwa sababu huwezi kujua mpinzani wako anaingia kwa mfumo gani au mbinu ipi,” alisema Nabi.

Kuhusu kikosi chake, Nabi alisema Shaban Djuma hakufanya mazoezi na timu kwa sababu ya kuugua mafua, lakini wengine wote waliobaki wako vizuri kwa ajili ya mchezo huo.

Aidha, Nabi aliwashukuru mashabiki wa Yanga kwa sapoti yao na kuwaomba mechi ya leo kuwa pamoja katika dakika zote 90 iwe mpira unakuwa kwao ama kwa wapinzania wao.

“Mashabiki wanatakiwa kuinga mbele, hata kama mchezaji wetu akipoteza basi

INAENDELEA UKURASA 23

# Robertinho aanza kuanika majembe yake

**Na Saada Akida**

KUFANYA vibaya kwa kikosi cha Simba msimu huu, kimeiamsha mapema klabu hiyo katika suala zima la usajili baada ya Kocha Mkuu Robertinho Oliveira, kuanza harakati za usajili huku akipendekeza katika kitabu chake jina la winga wa Vipers United, Mganda Milton Karisa, kuelekea msimu ujao.

Simba msimu huu imeshindwa kuchukua kombe lolote baada ya kutolewa kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kabla ya kutupwa nje pia katika hatua ya nusu fainali ya Kombe FA huku matumaini ya ubingwa wa Ligi Kuu Bara yakitoweka kutokana na kuzidiwa pointi saba na watani wao wa jadi, Yanga wakati huu zikiwa zimesalia raundi tatu kabla ya msimu kumalizika.

Taarifa za uhakika kutoka ndani ya uongozi wa Simba, zimeeleza kuwa tayari Robertinho ameshawasilisha kwa uongozi majina ya wachezaji anaowataka akiwamo Karisa ambaye amewahi kufanya naye kazi pale Vipers United.

“Robertinho ameshamaliza awamu ya kwanza ya majina ya wachezaji ambao anawataka kwa ajili ya msimu ujao na amefanya haraka kutokana presha kubwa ambayo ipo ndani ya timu baada ya kufanya vibaya.

“Miongoni mwa majina ambayo amekabidhi kwa uongozi yupo yule mshambuliaji wa Vipers ya Uganda kwa sababu moja ya maeneo anayotaka kuweka sawa ni la ushambuliaji na ikizingatiwa uwapo wa michuano mikubwa ambayo ipo mbele yetu,” kilisema chanzo chetu ndani ya klabu hiyo.

Alipoulizwa Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, kuhusu mpango huo wa usajili, alisema bado hafahamu majina ya wachezaji watakaosajiliwa, lakini akasisitiza usajili watakaofanya utakuwa wa kishindo kutokana na kufanya vibaya kwenye michuano yote msimu huu.

“Bado sijapewa taarifa za majina ingawa ni kweli mchakato

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >